epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatatu Juni 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581703
www.ippmedia.com
MWANGA WA J

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA 12

**WACHEZAJI 11 WENYE ASILI YA AFRIKA MATAIFA YA ULAYA**

## LISSU AHADHARISHA

# Viongozi wanaohongwa watatuuza huko mbeleni

- **Asema** CHADEMA kunyimwa viwanja vya mikutano ni ukiukwaji wa sheria... *Endelea ukurasa 2*



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu,akizungumza juzi na wananchi wa Manispaa ya Singida katika mfululizo wa ziara yake ya kutembelea majimbo yote ya uchaguzi ya mkoa wa Singida.
**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Wilaya tishio vifo vya wivu wa mapenzi hizi hapa

UKURASA 7

UKURASA WA 5

### POLISI: TUNAMHOJI MALISA KUMHUSISHA MBUNGE NA MAUAJI

JESHI la Polisi limeweka wazi sababu za kumkamata na kumsafirisha kutoka jijini Dar es Salaam hadi Kilimanjaro na...

UKURASA WA 5

### DIWANI AHOJIWA BARAZA LA MAADILI KISA TAMKO MALI NA MADENI YAKE

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imemfikisha mbele ya Baraza la Maadili...



UKURASA WA 18

### NEEMA TELE UJENZI KITUO KIPYA CHA TEHAMA

SERIKALI imesema imekubaliana na Korea kujenga chuo...



## MABINGWA MIREMBE...

# Wanafunzi wanaokamia masomo hatarini kupoteza kumbukumbu

UK.4

**MICHEZO** **YANGA YATENGA BIL. 24/- KUJIENDESHA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na Balozi wa Italia nchini, Marco Lombardi ambaye amemaliza muda wake, katika ofisi ndogo ya Waziri Mkuu Magogoni Jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Lissu ahadharisha "viongozi wanaohongwa, watatuuza"

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu ametahadharisha wananchi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu kuwa wasikubali kuchagua watu "wanaohongwahongwa" ili wasije wakauza Watanzania.

Alitoa hadhari hiyo juzi alipozungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika stendi ya zamani Manispaa ya Singida ikiwa ni mfululizo wa ziara yake ya kutembelea majimbo yote ya uchaguzi ya Mkoa wa Singida kwa ajili ya kuhamasisha wananchi hususani wanawake kujitokeza kugombea na kushiriki uchaguzi ujao.

"Tuweke watu imara, tusiweke watu wanaohongwahongwa, tafuteni viongozi ambao hawatatuuza. Yeyote anayehongwa atatuuza. Mtafute watu wasiohonga ili waongoze haya mapambano, tusipofanya hivyo hatutaweza," alisema Lissu pasi na kufafanua kwa undani suala hilo.

Hata hivyo, kutoa na kupokea hongo ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Lissu alisema kazi ya sasa, Oktoba mwaka huu na mwakani 2025 ni kuandaa wagombea kwa ajili ya udiwani, ubunge na urais na kwamba harakati za ukombozi zinamhusu kila mtu asiyependa alichodai "uchafu unaofanyika nchini".

"Nani wa kuwaambia wananchi tusimame hivi? Huo ni wajibu wa sisi viongozi wa vyama, hivyo ni lazima tuhakikishe tunatengeneza huo uongozi unaohitajika ili kukusanya nguvu na hatimaye kufanya mabadiliko," alisema.

Lissu, akizungumza changamoto waliyopata ya kutaka kunyimwa uwanja wa kufanyia mkutano, alisema wakurugenzi wa halmashauri lazima watambue kuwa viwanja vya shule na maeneo mengine ya wazi ni mali ya umma, hivyo kuvizuia vyama vya siasa hususani vya upinzani kuyatumia ni kutenda kosa kisheria.

"Hapa tunapofanyia mkutano (stendi ya zamani Singida) tulinyimwa na Ofisi ya Mkurugenzi licha ya kufuata taratibu zote ikiwamo kulipia, lakini nilipopata taarifa niliwaambia 'mkutano nitafanyia hapohapo ambapo mmetukataza au mjiandae kunipeleka mahabusu'," Lissu alisema.

Alisema kama tabia hiyo ya kuinyima CHADEMA maeneo ya kufanyia mikutano kwenye viwanja vya umma itaendelea, chama hicho kitakuwa kikilazimika kufanya mikutano hiyo ya hadhara katikati ya barabara ili wahusika waone adha itakayojitokeza ya kuzuia magari kupita.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Patrick Ole Sosopi, alisema hali ya maisha kwa wananchi imekuwa ngumu kiasi kwamba vijana na wazee wamekimbilia kucheza michezo ya kubahatisha (kubeti).

Alisema Watanzania lazima watambue kuwa suala la siasa si sawa na mchezo wa mpira wa kushabikia timu kubwa kama za Simba na Yanga, hivyo kunahitaji umakini wa hali ya juu kuhakikisha wanachaguliwa viongozi makini watakaopambana kuondosha umaskini.

Jana Lissu aliendelea na ziara yake katika majimbo ya Singida Kaskazini na Singida Mashariki, wilayani ya Ikungi.

# ...walalama kunyimwa uwanja kufanya mkutano Shinyanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Shinyanga Mjini kimelalamikia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Shinyanga kuwanyima uwanja kwa ajili ya kufanya mkutano wa hadhara.

Kimedai kuwa uwanja kiliomba mara nyingi umekuwa unatumika kwa mikutano mbalimbali.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi na viongozi wa CHADEMA walipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Mwenyekiti wa Chadema Jimbo la Shinyanga Mjini, Hamis Ngunila, alidai kuwa Juni Mosi mwaka huu waliandika barua kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuomba watumie uwanja wake kufanya mkutano wa hadhara Juni 7 mwaka huu.

"Tulipokea barua kutoka jeshi hilo iliyokuwa na majibu yaliyosema siku tuliyoomba uwanja huo kutakuwa na shughuli nyingine," alidai Ngunila.

Alisema kuwa baada ya kupokea majibu hayo waliandika barua nyingine ya kuomba uwanja huo ili wafanye mkutano wa hadhara Jumatano juni 12 mwaka huu, nayo wakapewa majibu kwamba uwanja huo kwa sasa hautatumiki tena kwa shughuli za kisiasa bali unatumika kwa shughuli za majeshi na za kiserikali, hivyo watafute uwanja mwingine.

"Majibu ambayo tumepewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupitia barua zao hizi mbili yana uwalakini -- mara uwanja utakuwa na shughuli nyingine, tukasogeza siku mbele wakajibu tena uwanja huo hautumike tena kisiasa.

"Hapa inaonesha kwamba katika Mkoa wa Shinyanga kuna ukandamizwaji wa Demokrasia," alidai Ngunila.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi, alisema wamesikitika kunyiwa uwanja huo ilhali vyama vingine vya siasa vimekuwa vinautumia kufanya mikutano ya hadhara.

"Ukiangalia barua hizi mbili za Zimamoto zina majibu tofauti Hapa inaonesha kuna kitu au wamepokea maelekezo kutoka juu.

"Hata Tundu Lissu tumeshuhudia amekuwa wakimnyimwa viwanja vya kufanya mikutano ya hadhara kwenye baadhi ya mikoa, inawezekana kuna mikakati inatengezwa chini kwa chini.

"Mbona mwaka jana tulifanya mkutano wa hadhara kwenye viwanja hivyo? Kwanini sasa hivi tuzuiwe hasa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa?

"Pamoja na zuio lao, sisi siku hiyo ya Jumatano ambayo ni Juni 12, tutafanya mkutano hapo watake wasitake, sababu zao hazina mantiki wala hazipo kisheria," alidai.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Shinyanga, Martin Nyambala, alithibitisha wamewazuia CHADEMA kufanya mkutano wa hadhara kwenye uwanja huo.

Alisema kwamba zamani uwanja huo haukuwa chini ya jeshi hilo, ndiyo maana ulikuwa unatumika kwa shughuli zozote, sasa upo chini yao.

Kamanda Nyambala alisema kuwa baada uwanja huo kuwa chini ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kuna utaratibu ambao umewekwa kuwa uwanja huo sasa utatumika kwa shughuli za kijeshi na za kiserikali tu, shughuli za kisiasa hazifanyika mahali hapo tena.

Kiongozi huyo wa jeshi hilo alishauri viongozi wa CHADEMA watafute uwanja mwingine kwa ajili ya kufanyia mikutano yao ya hadhara.

Kuhusu kusudio la CHADEMA la kufanya mkutano uwanjani huko licha ya zuio lililopo, Kamanda Nyambala alisema suala hilo lipo nje ya mamlaka yake, hivyo mamlaka zingine zitashughulika nao.

Akiwa mjini Singida juzi, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu alisema kuwa kama tabia hiyo ya kuinyima CHADEMA maeneo ya kufanyia mikutano kwenye viwanja vya umma itaendelea, chama hicho kitalazimika kufanya mikutano hiyo ya hadhara katikati ya barabara ili wahusika waone adha itakayojitokeza ya kuzuia magari kupita.

Alisema maeneo ya wazi ni mali ya umma na ni kosa kwa kiongozi yeyote kuzuia wanasiasa kuyatumia kwa shughuli za kisiasa ikiwamo mikutano ya hadhara.

HABARI KITAIFA

# Urejeaji wa hiari wakimbizi wa Burundi mwisho Desemba 2024

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

SERIKALI ya Tanzania imesema haitaendelea na uhamasishaji wa urejeaji wa hiari kwa wakimbizi kutoka Burundi walioko katika Kambi ya Wakimbizi Nyarugusu, mkoani Kigoma ifikapo Desemba mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni (pichani) alipotembelea kambini Nyarugusu kwa lengo la kujua hali ya urejeaji wakimbizi wa nchi hiyo.



"Hatuoni sababu ya kufanya uhamasishaji baada ya Desemba 2024 kama ambavyo tulikubaliana katika mkutano wa 24 wa pande tatu uliofanyika Novemba 2023 jijini Dar es Salaam na kuona kuwa Burundi ni nchi ambayo ipo salama na sababu zilizowafanya wakimbizi wakimbie nchini mwao hazipo tena," alisema.

Waziri Masauni alisema kuwa mapema mwaka 2025, serikali itawahoji wakimbizi 100,000 wa nchi hiyo ambao wanaoonesha kutokuwa na nia ya kurudi nchini mwao ili ijue sababu zao na kuzipima, kisha ifanye uamuzi kutokana na sababu hizo kama zinawapa sifa za kuendelea kuwa na hadhi ya ukimbizi au la.

Alisema jitihada hizo za serikali zisitafsiriwe kuwa nchi haiwapendi wakimbizi wa nchi hiyo bali ni njia ya kuwafanya kuwa huru na kutumia fursa zilizopo za ujirani mwema na fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuimarisha uchumi wa nchi yao.

Waziri Masauni pia aliagiza Jeshi la Uhamiaji mkoani Kigoma kuongeza mbinu za kukabiliana na tatizo la watu wanaoingia nchini kwa vibali halali vya ujirani mwema kisha kukiuka makubaliano na kuishi nchini kinyume cha sheria

Akiwa katika Mpaka wa Tanzania na Burundi huko Manyovu, wilayani Buhigwe, waziri huyo alisema haridhishwi na utendaji wa maeneo ya mipakani kutokana na raia wa Burundi kuingia nchini na kukaa bila kuwa na vibali na wengine kutozingatia muda wa kuisha kwa vibali vyao.

Alisema watu hao kwa sasa ni wengi nchini kuliko wale ambao serikali imekuwa inafanya taratibu za kuwarejesha nchini kwao, jambo ambalo lisipochukuliwa hatua za haraka litachangia kuiweka nchi katika hatari za kiusalama.

"Watu wanaingia kwa vibali vya ujirani mwema na hawatoki, tuna uhakika gani kama hawapewi vitambulisho vya taifa na vya mpigakura? Tunajuaje kama ni Watanzania au siyo Watanzania? Tunajua watu hao wana nia gani na nchi yetu? Je, tunajua wanafanya nini huko mitaani?" Waziri Masauni alihoji.

Akizungumzia hali ya urejeaji, Mwakilishi wa Serikali ya Burundi nchini, Theophile Ndarufatiye alisema kuwa tangu mwaka 2017 hadi Mei 2024 wakimbizi 1,076,316 wamerejea nchini mwao, akisisitiza kuwa idadi hiyo ni ndogo na hivyo kuna haja ya kushirikiana na Tanzania ili kuhakikisha kasi ya urejeaji wa hiari inaongezeka.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji mkoani Kigoma, Novat Dawson alithibitisha kuwapo changamoto ya watu kukaa nchini bila kuwa na vibali na kusema kuwa inasababishwa na ukosefu wa alama za usalama katika vibali vya ujirani mwema ambavyo vinatumika kusafiria.

"Vibali vya ujirani mwema havina alama ya kiusalama ya kudhibiti wanaoingia na kutoka.

Hata ukiviweka kwenye mfumo haviwezi kuingia kwa kuwa ni karatasi ambayo mtu amebandika picha yake, anagongewa muhuri na kuandikiwa kwa mkono, ikiwa haya ndio makubaliano ya ujirani mwema," alisema Kamishna Dawson.

Alisema kuwa kwa mujibu wa sheria, vibali vya ujirani mwema vinadumu kwa muda wa siku 14 ndani ya nchi husika na kwenda ndani ya nchi kwa urefu wa kilomita 10 kwa sababu za kibiashara.

Hata hivyo, kiongozi huyo alisema raia wa Burundi wamekuwa wanakiuka sheria hiyo na kwenda nje ya Mkoa wa Kigoma, hata kuifikia mikoa ya Dodoma, Tabora, Dar es Salaam na Zanzibar kwa shughuli za kilimo na biashara.

Kamishna Dawson alisema atazungumza na mamlaka za nchini Burundi kwenye vikao vya ujirani mwema ili kutafuta njia sahihi ya kuboresha vibali hivyo na kuongeza udhibiti kwa kuweka baadhi ya alama za kiusalama katika vitambulisho hivyo ili kuendeleza azma ya ujirani mwema ya kufanya biashara za mipakani na kuimarisha Soko la Afrika Mashariki.

Alitaja jitihada za kudhibiti raia hao wanaokiuka sheria na makubaliano ya ujirani mwema kuwa zinaendelea kupitia doria za mashambani, vyombo vya usafiri na sehemu za biashara. Kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Machi - Mei 2024 walikamata raia wa Burundi 1,365. Kati yao, 1,210 wamefikishwa mahakamani na wengine kurudishwa nchini kwao.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

MAKALA MAALUM

# Wanafunzi wanaokamia masomo hatarini kupoteza kumbukumbu

Na Christina Mwakangale



WATAALAMU bingwa na bobezi wa magonjwa, afya ya akili na mfumo wa fahamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, wameeleza namna ubongo unavyoathiriwa kutokana na maradhi na kusababisha mtu kupoteza kumbukumbu.

Mbali na tafsiri hiyo hasi kwa ubongo, pia wanaeleza uwezo wa kiungo hicho muhimu na injini ya mwili kilivyo na utaratibu maalum wa kupoteza kumbukumbu mbaya, ikiwa ni matokeo chanya kuulinda ubongo.

Pia wanaonya jamii, hasa wanafunzi kutoyakamia masomo, hususan msimu wa mitihani, wakisema ubongo unapotwishwa mzigo mkubwa, hushindwa kutenganisha kumbukumbu ipi itumike sasa na ipi baadaye na kuwasababishia kupata matokeo hasi.

Kwa nyakati tofauti katika mjadala uliopewa jina la 'Uhusiano Kati ya Kupoteza Kumbukumbu na Afya ya Akili', mabingwa hao wameuelezea ubongo kwa undani namna unavyotenda kazi.

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Damas Mlaki, akiwasilisha mada kuhusu kiungo hicho, anasema taaluma yake inahusika katika kutibu waliopata maradhi na kuathiri ubongo kama vile kiharusi na ajali.

"Huwa ninashughulika na waliopata kiharusi na kupata changamoto ya usikivu na kupoteza kumbukumbu au aliyepata ajali, kisha akapata athari kwenye ubongo na kubadili mwenendo wa kiungo hicho kitabia," anasema bingwa huyo.

Alisema yumo pia katika kufanya uchunguzi wa kisa chochote ambacho huathiri ubongo, walioumia kichwani na wenye kifafa na kuonesha mabadiliko ya fikra, tabia na mwenendo kulinganishwa na awali.

"Ninaona wazee maana tatizo hili huwakumba zaidi, lakini hata watoto na kundi lingine. Kozi ya taaluma hii niliipata Afrika Kusini, ni wachache wanaofikia hatua hii hasa kwa nchi kama zetu, kwa sababu hadi kuwa bingwa bobezi kuna shahada hata tatu unasomea, zikijikita eneo fulani tu la mwili," anasema.

**KUMBUKUMBU NI NINI?**

Bingwa mbobezi huyo katika ubongo anasema kumbukumbu ni kitu kinachohifadhiwa katika ubongo kwa namna mbalimbali, kama vile maneno, picha, sauti, matukio na hata hisia.

"Uwezo ukiwa duni wa kupata taarifa ambazo zimehifadhiwa ndio changamoto yaani kama huna uwezo kuzileta, kuhuisha taarifa, ni tatizo tayari katika ubongo.

"Ili utengeneze kumbukumbu lazima milango yako ya fahamu iwe imekamilika, kwa sababu milango mitano ya fahamu ndio lango la kuingilia matukio, hisia, picha, sauti na kuzifanya kuwa kumbukumbu.

Dk. Damas alisema iwapo kumbukumbu itahifadhiwa kama picha, ni lazima macho yawe na uono mzuri, kinyume chake kumbukumbu ya picha kwenye ubongo itaathiriwa.

Pia mlango wa fahamu sikio, anataja kuwa kiungo muhimu cha kupeleka taarifa kwenye ubongo na kuzitunza, na iwapo uwezo wa kusikia ni duni hakuna sauti itakayohifadhiwa.

"Ngozi, kumbukumbu zingine ni za hisia, labda ukigusa lazima ngozi itambue hata bila mguso, hiki ni kitu fulani, kwa hiyo ubongo utatunza taarifa kwa siku nyingine ukiguswa tu ubongo unatumbua ni mazingira fulani," alisema.

"Kabla hatujasema huyu mtu anapoteza kumbukumbu lazima tuchunguze milango yake ya fahamu ipo sawa? Macho, pua, ngozi, kinywa, masikio."

Bingwa huyo anazitaja aina ya kumbukumbu; kumbukumbu za matukio (episode memory); kumbukumbu za maarifa (semantic memory); kumbukumbu za ujuzi, utaratibu (procedure memory; kumbukumbu ya hali (condition memory).

Alifanunua kumbukumbu za matukio, anasema inajikita mtu kukumbuka vitu kadhaa kama vile siku ya leo mlo ulikuwa upi, alikwenda wapi, alifika kliniki na kwamba wenye shida katika ubongo huenda wasitambue kama wamekula au la.

"Kumbukumbu ya aina ya pili ni ya maarifa, mfano kukumbuka vitu vya kimaarifa uliyopewa ikiwamo darasani, ukumbuke mji mkuu wa Tanzania ni Dodoma au Uganda ni Kampala, miaka inapita lakini maarifa haya yametunzwa, kinyume chake ni tatizo.

"Aina ya tatu ambayo ni kumbukumbu inayotunzwa na ubongo ni ujuzi. Mfano ukishaelewa namna ya kuendesha gari, au kuandika hutumii tena kumbukumbu. Unaweza kutekeleza bila kufikiri na unaandika vitu vingi bila kufikiri," alisema Dk. Damas.

Magonjwa yakitokea katika mfumo mmoja huweza kuathiri eneo moja la kumbukumbu, na lingine lisiathirike. Kumbukumbu aina ya nne inahusiana na hali, huzuni, furaha.

"Aina hii iwapo itaathirika taarifa zitaathiriwa mtu hacheki, hana huzuni. Au labda uliwahi kutenda kitu kilikupa furaha sana, ulikutana kimwili na mpenzi wako, ile kumbukumbu haitakutoka na kila unapomuona unakumbuka, unahitaji tena.

Msongo wa mawazo baada ya janga ni tatizo, baadhi hushindwa kuchakata kumbukumbu na tukio likiisha huwarudia tena kama vile linatokea sasa."

Bingwa huyo anataja mbinu za kujikinga na namna ya kufanya ubongo utunze kumbukumbu, kuwa ni kufanya mazoezi ya kimwili na kiakili, lishe bora na kupata usingizi wa kutosha kwa zaidi ya saa nane.

"Kazi kuu ya usingizi ni kurejeaha kumbukumbu. Wanafunzi wanaokesha kusoma bila kuupa nafasi usingizi ni tatizo. Wanaweza hata wanachokisona wasikikumbuke katika chumba cha mtihani. Inahitaji ulale angalau saa nane kwa siku, ili juzihuisha kumbukumbu.

Mbinu nyingine na kutunza kumbukumbu ni kuupa ubongo mazoezi ya kiakili, kuangalia filamu, kusoma vitabu, gazeti, kucheza michezo ya asili kama bao, sababu unatumia fikra kumshinda mwenzio mnapocheza. Wazee wanaocheza bao wanarejesha kumbukumbu," anasema.

**UBONGO HUJIKINGA NA ATHARI**

Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka hospitali hiyo, Dk. Godwin Mwisomba anasema pamoja na jamii kuwa na dhana wanaopoteza kumbukumbu wanatafsiriwa kwa mtazamo hasi, bado kundi hilo huuponya ubongo.

Anasema kwa ambao wamepitia majanga, matukio ya kutisha maishani, kupoteza kumbukumbu kuhusu matukio hayo husaidia kupunguza mawazo mabaya na athari za kujirudiarudia kwa tukio hilo kwenye akili.

"Upotevu wa kumbukumbu wengi tunapokea kama hasi lakini kwa afya ya akili ni afya. Yaani ni afya mtu kuwa na upotevu wa kumbukumbu fulani.

Akipoteza kumbukumbu kwake ni afya na ni jema husaidia kumwondolea magonjwa yatokanayo na tukio fulani, mfano tukio la maporomoko ya udongo Hanang', Manyara mtu akishuhudia nyumba, ndugu wanapotea, mtu kama huyu akiipoteza kumbukumbu hii, ni afya."

Alisema ubongo hujitibu kwa mfumo wake wenyewe, ili kujiweka sawa usiathirike na mfululizo au mlundikano wa matukio mabaya na kusaidia jambo kusahaulika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Lawala, anasema jamii hasa familia, iache kufananisha uwezo wa ubongo baina ya mtoto mmoja na nduguze, kwani ni kawaida kutofautiana kutokana na ubongo ulivyoendelezwa.

"Utafiti unafanywa duniani kote, lakini inaonesha uwezo wa ubongo kati ya binadamu mmoja na mwingine hutofautiana, licha ya kuwa na umri sawa hata kama watoto ni wa familia moja. Utakuta mzazi anamsema vibaya mtoto mwenye uwezo mdogo hata kumnyanyapaa. Si sawa!" anaonya.

## Tanzania yatajwa orodha ya umaskini wa chakula

**Na Jenifer Gilla**

TANZANIA imetajwa ni miongoni mwa nchi 20 ulimwenguni ambazo watoto wake wanakabiliwa na umasikini wa chakula, hivyo kuwa hatarini kupata utapiamlo.

Hayo yamebainishwa katika Ripoti ya Lishe ya Watoto iliyotolewa mwezi huu na Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), ikionesha hali ya upatikanaji chakula kwa watoto chini ya miaka mitano.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa asilimia 22 ya watoto nchini wanakabiliwa na umaskini wa chakula kwa kiwango kikubwa na asilimia 59 katika kiwango cha kati, hali inayohatarisha ukuaji wao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, asilimia 27 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, sawa na watoto milioni 181 wanapata milo isiyozidi miwili kati ya minane inayotambuliwa na shirika hilo.

Kati ya watoto hao, milioni 64 wanaishi Kusini mwa Asia na milioni 54 Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikijumuisha nchi za Tanzania, Uganda, Afrika Kusini, Somalia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Misri.

Nchi zingine ni Afghanistan, Bangladesh, China, Côte d'Ivoire, Ethiopia, Ghana, India, Indonesia, Myanmar, Niger, Nigeria, Pakistan, Ufilipino na Yemen.

Miongoni mwa watoto hao, wanne kati ya watano hulishwa tu maziwa ya mama na au bidhaa za maziwa au chakula chenye wanga, kama vile mchele, mahindi au ngano; chini ya asilimia 10 hulishwa matunda na mboga na chini ya asilimia tano hulishwa mayai, nyama, kuku na samaki.

Inaelezwa katika ripoti hiyo kuwa mapato ya kaya si sababu pekee ya watoto kukosa mlo kamili kwa kuwa changamoto hii huwapata watoto walio katika kaya maskini na zisizo maskini.

Ripoti hiyo inatahadharisha kuwa vyakula visivyo na afya na vinywaji vinatumiwa na idadi kubwa, hivyo kuibua wasiwasi wa watoto wanaoishi katika umaskini mkubwa wa chakula.

"Nepal, kwa mfano ina asilimia 42 ya watoto wanaoishi katika umaskini mkubwa wa chakula, hutumia vyakula vyenye sukari, chumvi au mafuta mengi, na asilimia 17 hutumia vinywaji vitamu," inaelezwa katika ripoti hiyo.

Ripoti inataja baadhi ya sababu za wazazi kushindwa kuwapatia watoto wao milo sahihi na inayotambulika kimataifa kuwa ni vita ya Urusi na Ukraine na ugonjwa wa UVIKO -19 na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kukabiliana na utapiamlo wa watoto, UNICEF inashauri serikali na washirika kuwekeza katika hatua za kuboresha upatikanaji milo mbalimbali na yenye lishe kwa watoto na kumaliza umaskini mkubwa wa chakula kwa watoto.

# Polisi yasema inamhoji Malisa kumhusisha mbunge na mauaji

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

JESHI la Polisi limeweka wazi sababu za kumkamata na kumsafirisha kutoka jijini Dar es Salaam hadi Kilimanjaro na kisha kumhoji Mwanaharakati Godlisten Malisa (GJ).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Simon Maigwa, alisema jana kuwa Malisa anahojiwa ili kuthibitisha namna alivyomhusisha Mbunge wa Jimbo mojawapo la mkoa huo na mtu aliyefanya mauaji ya kikatili mwaka jana ya Beatrice Minja.

Novemba 12, 2023, Beatrice Minja, Mkazi wa Kijiji cha Mbomai Motamburu-Tarakea, wilayani Rombo alichomwa visu 25 na mtu aliyedaiwa kuwa mpenzi wake na baadaye kupoteza maisha wakati anapata Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) Desemba 27 mwaka jana.

"Hilo tukio ndio linalomhusisha mbunge (hakumtaja); na ndio maana tumemkamata (Malisa) kwa kum-connect (kumhusisha) mbunge na kitu ambacho hakina ushahidi. Ndiyo tumemkamata ili aje athibitishe haya," alisema.

Novemba 12, 2023, Beatrice Minja (40), mkazi wa Kijiji cha Mbomai Motamburu-Tarakea, Wilaya ya Rombo, alichomwa visu 25 na mtu aliyedaiwa

Malisa alikamatwa Juni 6 mwaka huu jijini Dar es Salaam na kupelekwa Kilimanjaro kuhojiwa. Baadaye Juni 7 mwaka huu aliachiwa kwa dhamana mkoani Kilimanjaro baada ya kuhojiwa na makachero wa polisi, akituhumiwa kwa makosa matatu anayodaiwa kutenda kupitia akaunti yake ya Instagram.

Zimo tuhuma za kutenda kosa la kutoa taarifa bila kibali kupitia mitandao ya kijamii.

Juni 8 mwaka huu, baada ya kuripoti Kituo Kikuu cha Polisi Moshi, Malisa alihojiwa na baadaye kuachiwa kwa dhamana.

Malisa baada ya kuachiwa, alisema misukosuko aliyoipata haitamrudisha nyuma kwenye harakati za kutetea haki wananchi kwa kile alichodai kuwa yuko sahihi na alichokifanya.



Mafundi Ujenzi wa Kampuni ya Synohyo Cooperation Limited kutoka nchini China wakiendelea na ujenzi wa Barabara ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu kutoka Gongo la Mboto kuelekea Posta kupitia Mnazi Mmoja kwa urefu wa Kilometa 23 ambapo tayari umefikia zaidi ya asilimia 83. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani afikishwa mbele ya Baraza la Maadili akituhumiwa kuvunja sheria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imemfikisha mbele ya Baraza la Maadili Yusuph Kitumbo, Diwani wa Cheyo, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kwa tuhuma za kushindwa kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni kwa miaka minne mfululizo.

Kikao hicho cha Baraza la Maadili kilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa chini ya Mwenyekiti wake, Jaji mstaafu Rose Teemba pamoja na Mjumbe wa Baraza, Peter Ilomo.

Wakili wa Serikali Hassan Mayunga alidai mbele ya baraza kuwa kitendo cha kiongozi huyo kushindwa kutoa Tamko la Raslimali na Madeni ni ukiukwaji wa Kifungu cha 9(1)(b) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Akitoa ushahidi mbele ya baraza hilo kwa upande wa mlalamikaji, Ofisa Uchunguzi Mwandamizi Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi, Halima Ramadhani Mnenge alidai kuwa hata baada ya kiongozi huyo kukumbushwa kwa njia ya barua kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya kumtaka atimize wajibu wa kisheria wa kuwasilisha tamko la rasilimali na madeni, alishindwa kufanya hivyo. Shahidi huyo alidai kuwa pamoja na kiongozi huyo kushindwa kuwasilisha tamko hilo kwa muda wa miaka minne mfululizo tangu mwaka 2020, hata alipowasilisha tamko lake hakuzingatia muda uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

"Mwaka 2015 alipochaguliwa kuwa Diwani wa Kata ya Cheyo, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, hakutoa tamko ndani ya siku 30 kama Sheria ya Maadili inavyomtaka, badala yake alitoa tamko hilo mwaka 2016 baada ya kukumbushwa kwa barua. Mwaka 2017 pia hakutoa tamko kwa wakati," alidai shahidi huyo mbele ya Baraza la Maadili.

Alidai kuwa tangu mwaka 2020 hadi 2023, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haikupokea Tamko lake la Rasilimali na Madeni.

Diwani huyo katika utetezi wake aliliambia baraza kuwa hakuwa na elimu yoyote kuhusu ujazaji matamko na hajawahi kupata mafunzo yoyote kuhusu Maadili ya Viongozi wa Umma. "Tangu nilipochaguliwa kuwa Diwani wa Kata ya Cheyo mwaka 2015, sijawahi kuhudhuria darasa lolote la masuala ya maadili," alisema.

Alikiri kuchelewesha uwasilishaji Tamko la Rasillimali na Madeni la mwaka 2015 na mwaka 2016.

"Tamko la mwaka 2015 na mwaka 2016 niliwasilisha kwa kuchelewa wakati matamko ya mwaka 2020 na 2021 niliyawasilisha kwa njia ya barua pepe," alidai.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Mwenyekiti wa Baraza alimweleza mlalamikiwa kuwa wamesikia utetezi wake na baraza litafanya uchunguzi na kutoa mapendekezo yake kwa mamlaka husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji, klabu msikurupuke kwenye usajili

**KWA** sasa kinachozungumzwa kwenye soka ni usajili wa wachezaji baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024 ambao tumeshuhudia Yanga wakitangazwa mabingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

Ikumbukwe Yanga na Azam ndio watakaoiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Simba na Coastal Union wakishiriki Kombe la FA baada ya kushika nafasi ya tatu na ya nne kwenye ligi.

Kumalizika kwa ligi duniani kote ndio kipindi cha dirisha la usajili kufunguliwa ili kuzipa nafasi timu kuboresha vikosi vyao, lakini pia kwa wachezaji kutafuta 'malisho' mengine.

Hiki ni kipindi ambacho wachezaji wanajiweka sokoni kwa ajili ya kusaka waajiri wapya hasa kwa wale ambao mikataba yao imemalizika au kukosa nafasi kwenye timu zao.

Kama ilivyo duniani kote, hata hapa nchini kipindi cha usajili kimeanza, tayari baadhi ya wachezaji wanahusishwa kutaka kujiunga na timu nyingine au kuongeza mikataba kwenye klabu zao za sasa.

Nipashe tunatumia fursa hii kuzikumbusha klabu na wachezaji juu ya usajili, kila upande ukubaliane na usajili wenye tija kwa manufaa yao na kwa manufaa ya soka letu.

Tukianza kwa upande wa wachezaji, ni kweli huu ni muda wa kusaka malisho bora zaidi, lakini pia waangalie na vipaji vyao, wasikubali kusaini mkataba kwenye klabu ambazo hawawezi kupata nafasi ya kucheza na kuonyesha vipaji vyao.

Kipaji na afya njema ndio mtaji wa mchezaji yeyote duniani, wachezaji watafute sehemu yenye malisho bora, lakini pia sehemu ambayo wataweza kupata nafasi ya kucheza na kuonyesha uwezo wao.

Deni Nkane, ni mchezaji mwenye kipaji, kipaji chake kilionekana kwenye klabu ya Biashara kwa kuwa timu hiyo ilimpa nafasi ya kukionyesha kwa maana walimpa nafasi ya kucheza mara kwa mara na ndipo hata Yanga walipomuona na kumsajili.

Hata hivyo upepo umekuwa mbaya kwake, na watu wameanza kusahau kipaji chake kwa sababu hapati nafasi ya kucheza ndani ya klabu hiyo, hii ni hatari kwa kipaji chake ikizingatiwa bado kijana mdogo.

Wachezaji waangalie mustakabali wao kabla ya kufanya maamuzi yoyote ya kuingia mkataba na klabu husika nje wasiangalie pesa peke yake. Soka ni ajira ya muda mfupi zaidi, mchezaji anaonekana 'Mzee' pindi anapofikisha miaka ya 28 na kuendelea, wanapaswa watumie vizuri vipaji vyao.

Klabu nazo ziepuke usajili wa mashinikizo na kukurupuka, ziangalie hasa mahitaji ya vikosi vyao kuelekea kwenye usajili.

Zisisajili wachezaji ambao hawatakuwa na tija kwenye vilabu na kujiongezea gharama za kuwalipa mishahara, ni kweli sio kila mchezaji atapata nafasi ya kucheza kwa sababu uwanjani wanaingia wachezaji 11 na wachezaji wanne wa akiba, lakini bado kuna sababu za kusajili wachezaji wanaowahitaji zaidi.

Hii itapunguza gharama kwa uongozi lakini pia itampa nafasi kocha wa timu kupanga wachezaji wake kutokana na ubora wa kila mchezaji, vilabu viepuke sajili za kukomoana na mihemko.

Kikubwa makocha wapewe nafasi ya kufanya maamuzi kwenye usajili, wao ndio wanajua kikosi kinahitaji nini na kwa wakati gani ili kufanya vizuri kwenye mashindano wanayoshiriki.

Ripoti wanazozitoa viongozi wa klabu wazitumie na wafanikishe kile ambacho makocha wanakitaka ili baadae waweze kumhukumu kocha kutokana na kile alichokifanya baada ya kutimiziwa kila kitu kwenye ripoti yake.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wajumbe Simba tangulizeni maslahi ya klabu, siyo yenu

**WAKATI** Simba ikifanya vibaya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, upande wa mwekezaji na wanachama walikuwa kimya.

Wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao walikuwa wakinung'unika, wakiwa na maswali mengi ya kujiuliza, kwa nini kikosi chao kinacheza vibaya, kina mapungufu, na hakishindi kwa 'swaga', bali papatupapatu, walikosa watu wa kuwaambia kitu.

Wakawa wanaulizana wenyewe kwa wenyewe bila kupata jibu, matokeo yake wakagawanyika na kugombana wao kwa wao.

Ni mtu mmoja tu angalau alikuwa anaweza kutoka na kuwafariji Wanasimba, naye ni Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally.

Ahmed ndiye aliyeonekana kuwa karibu na wanachama na mashabiki, akawa kiunganishi pekee kati ya timu, uongozi na wenye timu yao kwa maana ya mashabiki.

Mambo yaliendelea kuwa mabaya, lakini hakuna mjumbe yeyote aliyejitokeza kuelezea sababu ya timu hiyo kufanya vibaya.

Wote wako kimya na walionekana kama vile hawajui wajibu wao kwamba wanapaswa warudi kwa waliowaweka madarakani kuwaambia kila kitu kinachotokea.

Hawakujali manung'uniko, machungu na maumivu ya wanachama na mashabiki. Hata ligi ilipomalizika, bado walikuwa kimya. Wakati wenzao Yanga wakiwa wameitisha Mkutano Mkuu, wao waliendelea 'kuuchuna'.

Ndipo Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Klabu hiyo akaibuka na kuwataka wajumbe wote walio upande wake wajiuzulu.

Inasemekana wengine wamegoma. Baadhi ya wanachama wanaona isiwe tabu, wakawataka na wa upande wao kuachia ngazi kabla hawajachukua hatua za kikatiba.

Sasa ndipo tukaona wajumbe ambao siku zote walikuwa 'wameuchuna' wakijitokeza.

Ni kama walikuwa wamejificha kwenye mashimo. Cha ajabu badala ya kwenda kumaliza kiu ya wanachama na mashabiki kwa nini msimu huu timu imefanya vibaya, imekuwaje wamesajiliwa wachezaji ambao wanaonekana wana viwango vidogo, na kwa nini muda wote timu inafanya vibaya wao wako kimya, wao ametoka moja kwa moja na kuitisha kikao na viongozi wa matawi kuelekezea uwekezaji wa Mo, kasoro zake, na mambo mengine ambayo ukiyasikiliza utagundua kuwa wanachofanya ni kuhamisha ajenda, yaani waonekana kuwa wao wapo safi, tatizo lipo kwa Mo.

Mo huyu huyu ambaye ameipa Simba ubingwa misimu minne mfululizo, leo amegeuka na kuwa mbaya.

Mo ambaye anadaiwa kuwa hatoi pesa, lakini wajumbe hawataki kujiuzulu.

Unachojiuliza kama pesa hakuna, kwa nini wanang'ang'ania na imekuwa kwao ngumu kuwajibika?, ina maana wao ndiyo wanataka kutoa pesa za usajili?, wao ndiyo watakuwa na pesa za kuwalipa wachezaji mishahara?.

Ikumbukwe Simba kabla ya Dewji, ilikuwa ikipiga mechi za 'ndondo' ili kupata pesa za kujikimu.

Timu ilikuwa inafanya mazoezi kwenye Uwanja wa Kinesi maeneo ya Sinza, ikiwa haina hata mashabiki waliokwenda kuangalia mazoezi ndiyo wanaochangia pesa waliokuwa nayo ili zinunuliwe katoni za maji.

Nilidhani kama wana hoja za msingi, kwa nini wasiitishe Mkutano wa dharura wa wanachama wote, badala ya kusaka watu wachache tu ambao ni viongozi wa baadhi ya matawi, Dar es Salaam?.

Mimi nadhani wajumbe hawana hoja, na huku ni kutapatapa baada ya shinikizo kutoka kwa baadhi ya wanachama kuwa wajiuzulu, wameshindwa kuiongoza klabu.

Soka ni mchezo wa wazi, inaonekana kabisa Wajumbe na Bodi wamefeli, na hili limeelezwa na hata na mchezaji, Fondhoh Che Malone, na kocha wa makipa, Daniel Cadena ambao kwa nyakati tofauti wamesema tatizo la Simba lipo kwenye uongozi. Hawajasema mwekezaji. Na hii wala haihitaji elimu ya Chuo Kikuu kufahamu hilo.

Kumtupia lawama Mo ni kutapatapa kwa sababu Mo ameshaifanya Simba kuwa bora, lakini wao hawajawahi kuifanya kuwa hivyo tangu walipoteuliwa na wengine kuchaguliwa.

Hii inaonyesha kuwa wajumbe hawa wana maslahi binafsi na si kingine. Huwezi kung'ang'ania sehemu ambayo unasema fulani anafaidika na siyo wewe.

Mimi nawashauri kama kweli wapo hapo kwa maslahi wa Simba na si yao wajiuzulu kama walivyofanya wengine, kina Rashid Shangazi, Raphael Chageni, Hamza Johari, na Zulfikar Chandoo ambao wamekuwa wazalendo na kuweka mbele maslahi ya klabu.

Vinginevyo waitishe Mkutano Mkuu wa dharura ili wakawekane sawa mbele ya wanachama wote badala ya kutafuta kichaka cha kujifichia.

## HABARI KITAIFA

# Waishukuru serikali kupeleka mradi wa maji wa mil. 420/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Kijiji cha Kigoda, Kata ya Gwata, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha wameshukuru serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kuwapelekea mradi wa maji safi na salama.

Ni shukrani zilizotolewa jana kijijini huko, RUWASA walipomkabidhi mradi mkandarasi, Kampuni ya Lukedan Company Ltd atakayetekeleza mradi huo ambao ukikamilika utahudumia wananchi 934.

Kangale Julius na Kushoni Sembuli ni miongoni mwa wananchi walioshuhudia makabidhiano hayo ya mradi, wote walipongeza hatua hiyo na kusema kuwa sasa wanatumia maji ya kwenye lambo kwa matumizi ya nyumbani na mifugo.

Walisema mradi huo ukijengwa kwa kuzingatia muda uliopangwa, utawasaidia kuondokana na adha ya kutumia maji ambayo si safi na salama.

Awali akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kibaha, Debora Kanyika alisema kuwa kwa awamu ya kwanza mradi huo utaanza kutekelezwa katika Kijiji cha Kigoda.

Debora alisema chanzo cha maji cha mradi huo ni kisima kirefu chenye mita 150 na kina uwezo wa kutoa maji lita 9,500 kwa saa na kwamba katika mradi huo vituo 10 vya kuchotea maji vyenye koki mbili vitajengwa.

"Ofisi ya RUWASA Kibaha inapenda kuishukuru serikali kwa kuwezesha fedha za ujenzi wa mradi wa maji Kigoda Ngwale, mradi ambao unakwenda kupunguza changamoto ya upatikanaji maji safi na salama kwa wananchi na utaongeza upatikanaji maji katika wilaya hii," alisema.

Debora pia alitaja kazi zitakazofanyika katika mradi huo kuwa ni pamoja na ujenzi wa tangi lenye ujazo wa lita 100,000 juu ya mnara wa mita 12, mbaruti mbili kwa ajili ya kunyweshea mifugo, uchimbaji na ufukiaji mitaro na ulazaji wa mabomba mita 9,448.63.

Kazi nyingine ni pamoja na ununuzi wa pampu yenye uwezo wa kusukuma maji lita 7,000 kwa saa. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita, ukigharimu Sh. 420,821,057.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala ( kulia) akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas mara baada ya kumaliza mbio zake mkoani Mtwara makabidhiano hayo ya mwenge kutoka mkoani Mtwara na kuingia mkoani Ruvuma yamefanyika jana katika kijiji cha Sauti Moja kilichopo mpakani mwa mkoa wa Mtwara na Ruvuma. **PICHA: HAMISI NASRI.**

# Wilaya hizi tishio vifo vya wivu wa mapenzi

**Godfrey Mushi,** MOSHI

MAUAJI ya wenza yanatokana na wivu wa mapenzi yanazidi kuzitikisa wilaya tatu za Mwanga, Same na Moshi, mkoani Kilimanjaro, huku Jeshi la Polisi likieleza kuwa vifo vinane vilivyotokea hivi karibuni chanzo chake ni wanandoa kuendelea kuvumilia migogoro na vipigo.

Katika kipindi cha kuanzia Januari 2023 hadi Mei mwaka huu, yameripotiwa mauaji ya wenza wanane yanayotokana na wivu wa mapenzi mkoani humo. Hayo ni pamoja na ya kuchomwa kisu sehemu mbalimbali za mwili na kupigwa na kitu kizito.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Simon Maigwa, njia pekee iliyobakia ya kukabiliana na vifo ni wenza au watu waliopo katika uhusiano kutengeneza namna bora ya kuishi na kuacha kuiga wengine wanavyoishi.

"Ni lazima jamii ielewe kwamba wanapaswa kukubaliana namna walivyo na udhaifu wao. Yaani kukubaliana kwa yale wanayotofautiana, wapeane uhuru wa kuishi maisha apendayo kila mmoja na kukubali kuheshimiana.

Aliyataja mauaji hayo ni pamoja na la Mei 25 mwaka huu, mfanyabiashara Evagro Msele (43), aliyedaiwa kuuawa na mkewe Beatrice Elias (36) kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali mgongoni kutokana na kinachodaiwa wivu wa mapenzi.

Mei 8 mwaka huu, Mwamini Rashid (54), mkazi wa Kijiji cha Kiruru, wilayani Mwanga alidaiwa kuuawa na mumewe kwa kunyongwa hadi kufa kwa kutumia mtandio.

Kamanda Maigwa alieleza kuwa mwanamke huyo aliuawa baada ya kutokea ugomvi wa kifamilia uliochangiwa na kutopata mtoto kwenye ndoa yao.

Vilevile, Aprili 4, 2023, kuliripotiwa tukio la Donatha Macha (50), mkazi wa Kata ya Kirua Vunjo, wilayani Moshi, kuuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali usoni, kidogoni na mikono yote miwili.

Baada ya kuuawa, ilidaiwa kuwa mumewe alimchoma na kitu butu katika sehemu zake za siri kutokana na kiilichodaiwa wivu wa mapenzi.

Juni 9, 2023, kuliripotiwa pia tukio la mkazi wa Mbuyuni, wilayani Same, Noveni Msangi (33), kuuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali na watu watatu; wanaume wawili na mwanamke mmoja.

Chanzo cha mauaji ya Noveni kilidaiwa kuwa ni kutuhumiwa na mumewe kwamba si mwaminifu katika ndoa yao.

Februari 2, 2023, mkazi wa Kata ya Kirua Vunjo, wilayani Moshi, Fausta Tesha (26), alidaiwa kuuawa kwa kuchomwa na kisu kifuani, kifuani na kukatwa tumboni na mumewe ambaye pia alidaiwa kuua mtoto mwenye umri wa wiki mbili kwa kumkata tumboni na utumbo kutoka nje.

Ilidaiwa kuwa mumewe alikuwa anamtuhumu kupata ujauzito ambao si wake na wakati anarejea kutoka machimboni mkoani Tanga, alimkuta tayari ana mtoto.

Julai 29, 2023, Richard Zawadi (31), mkazi wa Kijiji cha Hedaru, wilayani Same, aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali mgongoni na kisha kupigwa na kitu kizito na mtuhumiwa Sendoro Mtera (20), ambaye naye alijeruhiwa na na wananchi na kisha kupoteza maisha akiwa Hospitali ya Wilaya ya Same.

Julai 31, 2023, mkazi wa Kijiji cha Kirima, Tarafa ya Kibosho, wilayani Moshi, Maria Mushi, alidaiwa kubakwa na hawara yake na kisha kuuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali katika sehemu mbalimbali za mwili wake kutokana na kile kinachoelezwa na Jeshi la Polisi kuwa ni wivu wa mapenzi.

Novemba 12, 2023, mkazi wa Kijiji cha Mbomai Motamburu, Tarafa ya Tarakea, wilayani Rombo, Beatrice Minja (40), alidaiwa kuuawa na mpenzi wake kwa kuchomwa visu 25 katika sehemu mbalimbali za mwili wake kutokana na tuhuma za kutokuwa mwaminifu katika uhusiano wao.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**






Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo akimkabidhi cheti mmoja wa wanafunzi 23 waliohitimu mafunzo ya cherehani kupitia mradi wa wezesha binti ulioko chini ya taasisi ya Panda Initiatives inayojihusisha na kuwawezesha wasichana na wanawake na makundi maalumu. Hafla hiyo ilifanyika Kivule jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Rehema Sanga. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Asafiri Km 1,300 kuteta na aliyekeketa mabinti 2,000

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga amelazimika kusafiri umbali wa zaidi ya Km 1,500 kutoka Dar es Salaam hadi Tarime, mkoani Mara, kukutana na Bhoke Ryoba aliyekuwa ngariba.

Bhoke (66), anadaiwa kutekeleza ukeketaji kwa mabinti zaidi ya 2,000 katika kipindi cha miaka 10 aliyofanya kazi hiyo.

Huyo ni mkazi wa Kijiji cha Masanga, Kata ya Nyamwale, wilayani Tarime. Aliachana na shughuli hiyo mwaka 2015 huku akikiri alifanya hivyo, akiamini alikuwa sahihi kwa mujibu wa mila zao.

Dk. Anna aliamua kumtembelea bibi huyo baada ya kupewa taarifa na Asasi ya Kupinga Ukeketaji (ATFGM) ya mkoani Mara, akitaka kujua sababu ya Bhoke kutekeleza ukeketaji ilhali ni kinyume cha sheria.

Akieleza kuhusu kutekeleza biashara hiyo, Bhoke alisema jamii ya Wakurya inaheshimu na kuenzi ukeketaji na endapo angeachana na shughuli hiyo mapema, kulikuwa na uwezekano wa kuuawa na jamii hiyo.

Alisema alikuwa anafanya hivyo ili kusaidia mabinti kuolewa bila shida na kujipatia fedha ambazo zimemsaidia kujenga nyumba mbili na kusomesha watoto.

"Gharama ya kulipia ukeketaji ni Sh. 10,000 na hiyo ni kwa miaka ya 2008 na kwa wakati huu gharama inafika mpaka Sh. 20,000. Kwa msimu wa ukeketaji huwa tunakeketa zaidi ya mabinti 200 na wazazi wao lazima walipie fedha na zinagawanywa kwa wazee wa mila na mangariba.

"Nilikuwa sijui kama kukeketa ni kosa kisheria, jamii ya huku wanaamini binti asipokeketwa anakuwa hajatimia, ndio maana hii mila bado inaendelea huku. Kwa kifupi, huu ni mradi wa mangariba kujipatia fedha," alisema Bhoke akiwa nyumbani kwake alipozungumza na Dk. Anna kuhusiana na ukatili huo.

Dk. Anna alionya kitendo cha baadhi ya mangariba kubadili ukeketaji kuwa mradi, akitaka jamii kutokutumia kama kivuli cha kujipatia fedha. Alisisitiza kitendo hicho ni ukatili wa kijinsia na kinakatisha ndoto za mabinti wengi.

"Jambo hilo limekuwa linasababisha madhara mengi ikiwamo kukatisha masomo, ndoa za utotoni, vifo kwa watoto hasa wakati wa kujifungua pamoja na kuchochea magonjwa mbalimbali," alisema Dk. Anna.

Mkoa wa Mara, hasa jamii ya Wakurya, umekuwa ukiendelea kuenzi mila ya ukeketaji kwa miaka ambayo inagawanyika kwa mbili na wamekuwa wakifanya maandalizi makubwa katika kutekeleza zoezi hilo ambayo huanza Agosti na ukeketaji hufanyika Desemba.


**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI) CONSULTANCY SERVICES FOR DESIGN AND SUPERVISION**

SICPA

**SICPA Tanzania** invites legally registered and experienced local consultants to submit their expression of interest for the ventilation and fire suppression systems detailed design, and supervision of construction works at Warehouse located Tazara -Dar es salaam.

Interested Firms are now requested to submit the following information.

- Company profile with firm background, physical address, official contacts (email & phone), organizational structure, director's, key staffs and their qualification and experience, area of experience
- Certificates of business registration
- Valid Tax clearance certificate
- Annual turnover for last 3 years
- Previous experience and clients similar to our requested consulting assignment.
- Any other necessary legal documents.
- The Consulting firm should be Licensed as Local consulting firm in the United Republic of Tanzania for past 3 years with a valid annual practicing certificate.

Submission should not be later than **21st June, 2024** at **16:00** via email to **tendersTZ@sicpa.com**

All companies will go through a screening and the successful applicant will be given opportunity to provide technical and financial proposals.


# AU yawatambua Samia, Ulega kinara kuendeleza uvuvi Afrika

**Na Maulid Mmbaga**

UMOJA wa Afrika (AU) na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) wamewatambua Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, kama vinara wa kuendeleza wavuvi wadogo Afrika.

AU iliwatambua viongozi hao kama vinara katika sekta hiyo wiki iliyopita wakati wa mkutano wa wavuvi wadogo Afrika, uliokuwa wa kwanza kufanyika barani, ukikutanisha wataalamu wa sekata ya uvuvi zaidi ya 1,000 kutoka mataifa mbalimbali Afrika.

Ofisa Uvuvi wa AU, Hellen Moepi-Guebama, alisema kufanyika kwa jukwaa hilo Tanzania ni uthibitisho wa jitihada za viongozi hao katika kuendeleza sekta ya uvuvi Afrika; lengo kuu la mkutano huo ni kuangalia namna nzuri ya kukomboa wavuvi wadogo.

"Tunatambua mchango wa Rais Samia kuanzisha na kusaidia wavuvi wadogo hasa kwa namna ya kutafsiri sera, miongozo, kanuni na mpango kazi wenye lengo la kusaidia sekta hii muhimu ya uvuvi barani Afrika.

"Tanzania kwa kupitia jitihada za Rais Samia, tumeshuhudia mkutano mkubwa wa wavuvi wadogo wenye lengo la kukusanya maoni ya wavuvi yatakayokwenda kufanyiwa kazi katika Mkutano wa Kimataifa utakaofuata Italia," alisema Hellen.

Alisema AU itaendelea kusimamia na kuhakikisha sera na miongoza iliyowekwa inatekelezwa na kuweka mikakati ya kuendeleza Mpango wa Uchumi wa Bluu kwa kuwa na mkakati maalum wa kukuza sekata ya uvuvi Afrika.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Tipo Nyabenyi, alisema "Italia mwaka 2023, Waziri Ulega aliahidi Tanzania kuandaa mkutano huu, ambao leo tunaona umefanikiwa kwa asilimia kubwa. Haya ni matunda ya serikali ya Rais Samia ambapo tunaona ni mwendo mzuri katika sekta hii ya uvuvi mdogo."

Alisema endapo sekta ya uvuvi mdogo itaendelezwa na kupewa ushirikiano, jamii itanufaika kwa kuwa sekta hiyo inatumika pia kama chanzo cha chakula na mapato cha watu na taifa.

Alisema jukwaa hilo linatoa fursa kwa wadau kushiriki mawazo mbalimbali ikiwamo changamoto kubwa wanazokutanazo kama mabadiliko ya tabianchi na kwamba wataendelea kufanya majadiliano na wadau wengine katika kuona namna bora ya kukuza na kuendeleza sekta hiyo.

"Tusikilize sauti za wavuvi na mkutano huu utakuwa ni taswira ya kudumu, katika kushughulikia matatizo ya wavuvi, na ninampongeza Waziri wa Uvuvi, Ulega leo tumeona hili limefanikiwa hongera sana," alisema Dk. Tipo.

Vilevile, alisema wavuvi wadogo wengi wanategemewa na familia zao katika suala la chakula, uchumi na maendeleo ya kijamii licha ya changamoto zinazowakabili, na FAO itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuwasaidia wavuvi Afrika.

Pia alisema wanapaswa kushirikiana kuonesha changamoto zilizoko katika sekta hiyo na kuzipatia suluhu kwaajili ya kulinda na kuchochea maendeleo katika uvuvi mdogo Afrika.

# TAWIRI yaweka mkakati kuvutia uwekezaji kwenye wanyamapori

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), imeweka mkakati wa kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii, baada ya kuanzisha kampeni maalum ya kutoa ushauri elekezi kwa kampuni za ndani na nje ya nchi zinazotaka kufanya biashara hiyo.

Kampeni hiyo, inalenga kuvutia uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori (zoo), matibabu ya wanyamapori, ufugaji bora wa nyuki na huduma mahususi ya kutoa elimu ya kisayansi juu ya wanyamapori.

Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI, Dk. Eblate Mjingo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye maonyesho ya kimataifa ya 'Karibu Kili Fair' 2024 yanayofanyika Jijini Arusha. Alisema taasisi hiyo imeanza kukaribisha wadau hao pamoja na mambo mengine kupata elimu juu ya mchango wa tafiti za wanyamapori katika kukuza utalii.

"Tunatoa ushauri wa kitaalamu (consultancy) wa uwekezaji kwenye utalii, uanzishaji wa mashamba ya wanyamapori (zoo), matibabu ya wanyamapori pamoja, ufugaji bora wa nyuki na huduma kisayansi juu ya wanyamapori (scientific talks).

"Tumeamua kufanya haya, kwa sababu maonyesho haya ya Karibu Kili Fair yamejikita kuendelea kukuza na kuimarisha utalii."

Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni ya Karibu Kili Fair, Dominic Shoo, alisema maonyesho hayo yamewakutanisha wanunuzi zaidi ya 600 wa bidhaa mbalimbali za utalii kutoka nchi 42 duniani, na wadau wa utalii 468 kutoka nchi 37.

Akifungua maonyesho hayo, Waziri wa Malisili na Utalii, Angellah Kairuki, alisema maboresho yaliofanywa na serikali katika sekta hiyo, yamechangia ongezeko la idadi ya watalii wa nje ya nchi na wa ndani, wanaotembelea vivutio vya utalii.

"Mazingira bora ya biashara kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi yamekuwa na tija kubwa katika sekta ya utalii tumeona idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi wakiongezeka kila siku.Nataka niwahakikishie kwamba serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta hii muhimu kwa taifa,"alisema Waziri Kairuki na kuongeza:

"Sekta ya utalii hapa nchini inachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.2 huku ikichangia asilimia 25 ya fedha za kigeni, lakini mafanikio yote haya yanatokana na ushirikiano mzuri wa serikali na sekta binafsi."

Kwa mujibu wa Waziri Kairuki, maonyesho hayo ya kimataifa Karibu Kili Fair, yana tija kubwa kwa kuwa yanawakutanisha watoa huduma za utalii nchini na wanunuzi wa bidhaa mbalimbali za utalii ikiwemo safari na hoteli.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza Dk. Jumaa Mhina kushoto akipewa maelezo na Mjasiriamali wa Kikundi cha Mbomole Spices, Dastan Daffa katika namna ya kutumia bidhaa za mazao ya viungo mara baada ya kuwasili katika banda la maonesho ya biashara na utalii la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza yanayoendelea katika viwanja vya shule ya sekondari ya Usagara iliyopo Jijini Tanga, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TARURA yajenga kilomita 127 za barabara Msomera

**Na Godfrey Mushi,**
HANDENI

HATIMAYE Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), amemaliza kilio cha wananchi wa jamii ya kifugaji ya kimasai, waliohamia kwa hiari katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, baada ya kufungua kilomita 127 za barabara za changarawe.

Wananchi hao ni wale waliohama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kupisha shughuli za uhifadhi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, baada ya kuzuru eneo hilo, Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff, alisema wamelazimika kupiga kambi katika kijiji hicho kilichoko Kata ya Msima, kutafuta ufumbuzi wa kero hiyo, ili kutekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"Tayari tumefungua barabara hizo katika Kijiji cha Msomera, ili kurahisisha shughuli za kijamii na kiuchumi, kwa wananchi wa maeneo hayo.

Zaidi alifafanua, 'Hili ni takwa na jukumu la kisheria la TARURA. Wakala utahakikisha unatekeleza maelekezo mbalimbali ya Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na serikali yake, ili kuchochea fursa za kiuchumi na kijamii katika maeneo wanayoishi."

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa TARURA, Mkoa wa Tanga, George Tarimo, alisema wamefamikiwa kufungua barabara hizo, ambazo hazikuwepo tangu nchi ilipopata uhuru.

"Tumefungua kilomita 137, lakini tuna zaidi ya kilomita 600 ambazo zinahitaji kufanyiwa matengenezo. Tunafanya matengenezo kutokana na fedha ya bajeti, bajeti ya mwaka huu 2024/25 kwa upande wa Handeni tumepitishiwa bajeti ya Sh. bilioni moja, kwa ajili ya kufungua barabara Kijiji cha Msomera," alisema Tarimo.

lbert Msando, alisema serikali kwani kipinda cha miaka mitatu, zaidi ya kilomita 180 za barabara zimefunguliwa, ambazo hazikuwepo kabisa kwa sababu eneo hilo lilikuwa pori tengefu.

Akizingumzia mradi huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Msomera, Martin Oleikayo, alisema awali walikuwa na barabara moja tu ya kutoka Handeni mpaka kijijini hapo, ambayo ilikuwa imeharibika vibaya na ilikuwa haipitiki.

# Chanzo kuongezeka udumavu chatajwa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

DIVISHENI ya afya na lishe ya Mkoa wa Manyara, imetaja moja ya kiini kinachosababisha ongezeko la udumavu katika maeneo mbalimbali mkoani humo, kunachangiwa na wazazi au walezi, kupuuza kinga tiba ya minyoo tumbo kwa watoto.

Mratibu wa Huduma za Matibabu kutoka Ofisi ya Mkuu wa mkoa huo, Dk. Mandala Adam, alisema jana katika mahojiano yake na Nipashe kuwa, watoto ambao hawapati kinga tiba wanaweza kupata udumavu na kushindwa kufundishika darasani.

Dk. Mandala alisema minyoo hiyo ikienda kwenye tumbo inashindana na mtoto, na ikiwa mingi chakula hakiwezi kumeng'enywa na hivyo kuhatarisha afya na ukuaji wa mtoto.

Alisema minyoo hatari ni aina ya hookworm, ambao wanapozidi tumboni kwa mtoto, uwezekano wa kutengeneza damu ni mdogo, ndio maana wengine hulazimika kuongezewa damu.

"Minyoo ikiwepo tumboni inaweza kuziba utumbo mpaka mtoto akafanyiwa upasuaji wa utumbo,"alisema Dk. Adam.

Alisema watoto wachanga siyo rahisi kupata minyoo maana mama anapaswa kunyonyesha kwa miezi sita mfululizo bila kumpa kitu chochote.

Kwa upande wake, Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, alisema minyoo ya tumbo inafyonza viini lishe, hasa kwa mama mjamzito na mtoto vilivyopo kwenye vyakula.

"Kuna mahusiano makubwa sana kati ya kupungua uzito na uwepo wa minyoo ya tumbo kwa mjamzito na mtoto madhara yake ni upungufu wa damu na kuongezeka kwa uzito ni nadra sana kwa mtoto,"alieleza Dalushi.

Kadhalika, Dalushi, alisema mzazi anaweza kumlisha mtoto ila viini lishe vikawa vinaliwa na minyoo na kuathiri ukuaji wa mtoto.

"Ili kukabiliana na hali hiyo alisema serikali mkoani humo imeanzisha wiki ya Afya na lishe ambayo inafanyika kila mwezi Juni na Desemba kila mwaka kuanzia tarehe moja hadi tarehe 30,"alisema.

Vilevile ofisa huyo alisema kwa mwaka huu, wanatarajia kuwafikia watoto 294,857 ambapo watoto chini ya miaka mitano watakuwa ni 256,480.

Kwa mujibu wa Dalushi, dhana ya udumavu kinachoanza kudumaa ni ubongo na chakula ndicho kinatengeneza ubongo hivyo mtoto akishambuliwa na minyoo ukuaji wa ubongo unaathirika zaidi.

"Mtoto minyoo ikimpunguzia hamu ya kula inampungizia makuzi yake na athari mojawapo ni kutokuelewa darasani,"alisema.

Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, James Mleli, alisema mnyoo mmoja anaweza kunywa damu milimita tano mpaka saba, hivyo kuathiri mtoto anayekuwa na minyoo ya tumbo.

Mleli alisema minyoo ikiwa mingi tumbo linajaa na hatimaye mtoto anadumaa kwa kuwa akiwa na minyoo anapoteza hamu ya kula na minyoo ndio inakula badala yake.





# Baba mbaroni kwa kumuunguza mtoto wa kambo kwa maji moto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Mtaa wa Shunu, Kata ya Nyahanga, wilayani Kahama Simon Hamisi (27), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuunguza kwa maji ya moto mtoto wake wa kambo jina limehifadhiwa, kwa kile kilichoelezwa ni ugomvi na mkewe, Elizabeth Mathias (24).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo Juni sita mwaka huu, majira ya saa mbili usiku katika mtaa tajwa hapo juu, mtoto huyo alikuwa kando ya jiko akiota moto kabla ya kukutwa na tukio hilo.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni baba huyo kuwa amelewa na kuleta vurugu kwenye familia yake, iliyopelekea kupiga teke sufuria la maji ya moto lililokuwa jikoni na kumwagikia mtoto huyo.

Sio sahihi kwa wazazi kutumia ulevi na kwenda kufanya vurugu kwenye familia, wanaoumia ni wanawake na watoto, kwa kitendo hiki cha ukatili kilichofanyika, sitakivumilia nitahakikisha mhusika anafikishwa mahakamani, ili iwe fundisho kwa wazazi wengine wenye tabia kama hizi," alisema Magomi.

Akisimulia tukio hilo, Mama mzazi wa mtoto huyo, Elizabeth Mathias, alisema ilikuwa majira ya saa mbili usiku wakati akichemsha maji jikoni ghafla aliingia mumewe na kuanzisha mzozo na kulipiga teke jiko lililokuwa na sufuria la maji ya moto na kumwagukia mtoto wake ambaye alikuwa amekaa karibu na jiko akiota moto.

"Ilikuwa usiku majira ya saa mbili, ghafla aliingia mume wangu na kuanzisha ugomvi, ndipo alilipiga teke sufuria lililokuwa jikoni lina maji ya moto na mtoto wangu alikuwa pembeni ya jiko hilo anaota moto maji hayo yalimmwagikia, nilipiga kelele kuomba msaada kwa majirani zangu, ambao walikimbia polisi kutoa taarifa na kupewa PF3, tulimkimbiza hospitali kwa ajili ya matibabu zaidi maana hali ilikuwa mbaya,"alisema Elizabeth.

Alisema hakuwahi kuwa na ugomvi wowote na mme wake, wala kumbagua mtoto wake huyo na alimpenda na kumhudumia mahitaji yote vema, lakini siku hiyo ilichangiwa na ulevi kwani alikuwa amelewa, huku akiomba serikali kumsaidia kupata matibabu kwa sababu fedha aliyonayo haikidhi mahitaji na amenunua dawa.

Aidha, Eliza aliwasihi wazazi wanzake kuacha kunywa pombe, kisha kufanya vurugu kwenye familia zao kunaleta matatizo ambayo wanaoumia ni watoto, huku akiliomba jeshi la polisi kuangalia namna ya kumsamehe mumewe kwa sababu ni tukio lake la kwanza kulitenda kwenye familia yake.

## Taarifa mapato na matumizi kikwazo kwa maendeleo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

IMEBAINISHWA kuwa suala la wenyeviti wa mitaa,watendaji wa vijiji na Kata kushindwa kusoma taarifa za mapato na matumizi, kwa wananchi kumesababisha mikanganyiko inayopelekea kuwepo kwa migogoro ya mara kwa mara ndani ya jamii.

Migogoro hiyo ni kwenye miradi ya maendeleo, ambayo inatekelezwa katika maeneo husika.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro wakati wa mkutano wa hadhara uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi katika Kata ya Solwa.

Katika ziara hiyo alibaini kuwa malalamiko mengi yanatokana na watendaji wa vijiji, kata na wenyeviti wa mitaa na vitongoji kutokusoma mapato na matumizi.

"Ninawaagiza watendaji na wenyeviti wa vijiji na mitaa,muanze kuwasomea wananchi mapato na matumizi, ili kuepusha migogoro hasa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo,"alisema Mtatiro.

Aidha, aliwataka watumishi wote wa serikali wilayani hapo, kutekeleza majukumu yao kwa weledi katika kuwatumikia wananchi, na kuwapatia huduma bora na siyo kusubiri msukumo kutoka kwa viongozi ngazi ya juu.

Baadhi ya wananchi wa Solwa waliwalaumu viongozi wao kwa kushindwa kusomea wananchi mapato na matumizi, huku wakitaja kero kubwa ambayo inawakabili kwa sasa ni ubovu wa miundombinu ya barabara.

## Wanaoshiriki UMITASHUMTA waonywa kutumia dawa za kulevya

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imewataka wanafunzi na walimu wanaoshiriki mashindano ya UMITASHUMTA Taifa, kutojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya.

Wito huo umetolewa na Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kanda ya Kati, Mzee Kasuwi, alipokuwa akitoa elimu ya madhara ya dawa za kulevya kwa walimu na wanafunzi.

Alisema dawa za kulevya ni hatari sana kwa afya za wanamichezo, ustawi wao na jamii kwa ujumla, hivyo akawataka kutojihusisha kwa namna yoyote ile na matumizi ya dawa hizo,wala wasikubali kushawishiwa na mtu yeyote.

Alisisitiza mashindano hayo ya Umoja wa Michezo na Taalumu kwa Shule za Msingi, yanayoshirikisha wanamichezo zaidi ya 4,000, ni fursa muhimu ya kuinua vipaji na kuviendeleza bila kuathiriwa na dawa hizo.

"Dhamira ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona wanamichezo wanafikia ndoto zao, hivyo elimu hiyo ni muhimu sana kabla ya kuanza michezo, ili kuwapa uelewa wa madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo,"alisema Kasui.

Alisema utoaji elimu ni moja ya mikakati ya Mamlaka hiyo,ikiwa ni kuelekea kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Matumizi ya Dawa za kulevya Duniani, ambayo Kitaifa yatafanyika Jijini Mwanza mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa upande wake, Ofisa wa mamlaka hiyo, Christian Mbwasi, aliwataka wanafunzi wote wanaoshiriki mashindano hayo, kutokubali kula au kunyweshwa kitu chochote wasichokifahamu wakati wote wa mashindano hayo.

Aidha, aliwataka wawe mabalozi wazuri kwa wenzao ikiwemo kuwakataza kutumia dawa hizo punde wanapowaona wakijiingiza katika makundi mabaya yanayotumia dawa hizo na watoe taarifa endapo wataona viashiria vya vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa mashindano hayo, Ernest Hinju, aliwataka washiriki wote kuonesha uzalendo, nidhamu na utii wakati wote wa mashindano hayo na kusisitiza kuwa hawatasita kuchukua hatua za kinidhamu kwa yeyote atakayeenda kinyume.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Alliance One, Ephraim Mapore (wapili kushoto) akikagua soko la tumbaku mkoani Tabora . Watatu kushoto ni Mkurugenzi wa Uzalishaji wa kampuni hiyo, David Mayunga.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC Mboni awaonya watumishi kuomba fedha kwa wachimbaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita amewataka baadhi ya watumishi wa idara ya mapato kuacha tabia ya kuwaomba msaada wa kifedha wachimbaji walio maeneo hayo, pindi wanapopata shida ya ada ya wanafunzi, misiba na sherehe, jambo ambalo linapelekea kushindwa kutimiza wajibu wa kikazi.

Mhita aliyabainisha hayo wakati wa ziara yake, kwenye Mgodi mdogo wa Mwabomba uliopo kijiji na Kata ya Mwabomba Halmashauri ya Ushetu, baada ya kuwepo kwa malalamiko juu ya wachimbaji kushindwa kulipa ushuru wa mawe yanayosadikiwa kuwa na madini na kuisababishia halmashauri kukosa mapato yake.

Alisema baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu wamewageuza wachimbaji wa madini, kuwa sehemu ya kitega uchumi cha kujipatia fedha, za kukidhi shida zao mbalimbali, hali inayosababisha serikali kuendelea kukosa mapato ya ushuru unaotakiwa kutozwa kwa kila mfuko unaozalishwa.

Mhita alisema serikali kupitia wizara ya madini, chini ya Waziri Antony Mavunde, imeendelea kutengeneza mazingira wezeshi yatakayomsaidia mchimbaji kuchimba madini pasipokuwa na vikwazo vyovyote, na kwamba linapoibuka suala la kuwatwisha majukumu ya ada ni kusababisha wakwepe kulipa ushuru uliopo kisheria.

"Niwatake wachimbaji wangu, pale mnapopata watumishi wa namna hii kutaka fedha kwa lengo la kujinufaika wao binafsi, mnipe taarifa kupitia simu yangu ya mkononi nami nitawashughulikia kwa mujibu wa sheria, tunataka watumishi ambao watasimamia vema suala la ukusanyaji wa mapato na siyo vinginevyo,"alisisitiza Mhita.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Mhandisi Joseph Kumburu, alisema awali ushuru wa Sh.2,000 kwa kila mfuko ulikuwa juu ukilinganisha na maeneo mengine,ambayo wanatoza Sh.1,000,ila kwasasa wanatoza kiasi sawa na wengine, ikiwa na kuhakikisha mapato ya serikali yanakusanywa vile inavyotakiwa.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 11 WENYE ASILI YA AFRIKA MATAIFA YA ULAYA UK. 12-13




# WACHEZAJI KUMI WANAOWEZA KUMFUATA MOURINHO FENERBAHCE

**ISTANBUL,** Uturuki

NI rasmi Jose Mourinho ndiye kocha mkuu mpya wa Fenerbahce.

Mreno huyo alikabidhiwa mikoba ya kuwa bosi mpya wa wababe hao wa Uturuki siku ya Jumapili, jambo lililofurahisha mashabiki wa timu hiyo inayotumia rangi ya bluu na njano.

Ligi Kuu ya Uturuki inajulikana kwa kuwa kitovu cha wachezaji wenye vipaji bora zaidi duniani na kumwongeza Mourinho kwenye mchanganyiko huo kunaboresha mpango wa aina hii.

Hapa tunawaangalia wachezaji 10 wanaoweza kumfuata Mourinho.

**1. Romelu Lukaku**

Mourinho tayari amemfundisha Romelu Lukaku katika klabu za Chelsea, Manchester United na AS Roma, akimsajili kwenye timu mbili za mwisho.

Mgombea urais wa Fenerbahce, Aziz Yildirim amemtaja Lukaku pamoja na Paulo Dybala na Anderson Talisca kuwa wachezaji watatu ambao klabu hiyo itatafuta kuwasajili iwapo atachaguliwa tena.

**2. Willian**

Mourinho anapenda winga ambaye anarudi nyuma. Willian ndiye aliyekuwa akifanya hivyo katika kipindi chake cha pili pale Chelsea.

Baada ya kuondoka Stamford Bridge, Mourinho anasemekana bado alimtaka Mbrazil huyo Manchester United na kisha Tottenham Hotspur. Huku Willian akikaribia kuondoka Fulham, usishangae kumuona akitua Fenerbahce msimu huu wa joto.

**3. Cedric Soares**

Hakuna uhusiano wowote wa awali kati ya Mourinho na Cedric Soares ambao tunaujua.

Lakini beki huyo wa kulia ni shabiki mkuu wa Mourinho na anaweza kusajiliwa katika Ligi Kuu ya Uturuki.

**4. Joel Matip**

Labda kituo hiki kingekuwa cha kuchelewa sana kwa Joel Matip, ambaye alionekana mchanga kwa miaka mitano kabla ya jeraha la mwisho wa msimu uliopita.

Lakini baada ya mkataba wake na Liverpool na katika kutafuta klabu mpya, anaweza kuwa mchezaji ambaye Mourinho atamtaka kwa ajili ya kujenga msingi katika klabu ya Fenerbahce.

**5. Anthony Martial**

Je, kumewahi kuwa na jina kubwa kama hilo ambalo nafasi zake za kwenda Fenerbahce zilizidishwa na kocha mkuu kujiunga?

Anthony Martial alihusishwa kwa mara ya kwanza na wababe hao wa Uturuki miezi kadhaa iliyopita. Uvumi huo labda utakauka kidogo sasa ukizingatia uhusiano wake na Mourinho.

**6. Angelo Ogbonna**

Angelo Ogbonna ana umri wa miaka 36, mkataba wake unamalizika msimu huu wa joto, ameshinda mataji matano katika maisha yake ya soka na kucheza mechi 492 za klabu.

Anafaa kuwa sehemu ya timu ya Mourinho pale Fenerbahce.

**7. Ashley Young**

Mashabiki wa Everton wameonekana kuwa na furaha na Ashley Young, ambaye hajapungua hata kidogo akiwa na miaka 38.

**8. Matt Doherty**

The Wolves wa zamani wangekuwa wamejaa wachezaji wanaowasha tu nafasi ya kucheza chini ya Mourinho huko Fenerbahce.

Siku hizi, uteuzi umepungua hadi kwa Matt Doherty, ambaye tayari amechezea Mourinho huko Tottenham na alisifiwa huko Spurs kwa vibe yake ya chumba cha kubadilishia nguo.

**9. Neal Maupay**

Neal Maupay na Mourinho nyumba mbili bora zaidi za mchezo. Pamoja katika Fenerbahce.

## ISIKUPITE

YANGA ndio timu pekee kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika hivi karibuni kushinda mechi zote 15 za nyumbani, mechi hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kutetea ubingwa wao kwa mara ya tatu mfululizo.

## Extra Time

# WACHEZAJI 11 WENYE ASILI YA AFRIKA WATAKAOCHEZEA MATAIFA YA ULAYA

**BERLIN,** Ujerumani

MIONGONI mwa wachezaji waliochaguliwa kucheza michuano ya soka ya Mataifa ya Ulaya (Euro 2024) baadhi yao wana asili ya Afrika na wangeweza kucheza Kombe la Mataifa ya Afrika katika nchi zao za asili kama wangetaka.

**Hii hapa ni orodha ya majina ya wachezaji 11 wenye asili ya Afrika watakaoshiriki Euro 2024, kuanzia Juni 14 hadi Julai 14 nchini Ujerumani.**

### Brice Samba (Ufaransa-Congo)

Brice Samba, kipa wa RC Lens, aliitwa kwenye timu ya Ufaransa kwa mara ya kwanza na kocha Didier Deschamps Machi 2023.

Kipa namba mbili wa Ufaransa alizaliwa na wazazi kutoka Congo Aprili 25, 1994 huko Linzolo, kilomita 20 kusini mwa Brazzaville, mji mkuu wa Jamhuri ya Congo.

Alifunzwa katika klabu ya Le Havre na alicheza Marseille, Caen na Nottingham Forest ya Ligi ya England na sasa anachezea RC Lens ya Ufaransa tangu 2022.

Samba mwenye miaka 30 ambaye hakuwahi kuitwa kabla, atacheza katika mashindano ya kimataifa kwa mara ya kwanza kama kipa namba mbili nyuma ya Mike Maignan.

### Antonio Rüdiger (Ujerumani - Sierra Leone)

Antonio Rüdiger moja ya mabeki bora duniani, alizaliwa Ujerumani mwaka 1993, na mama wa Sierra Leone ambaye alikimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe na baba Mjerumani.

Rüdiger alicheza mechi yake ya kwanza ya Bundesliga akiwa na Stuttgart Januari 19, 2012 akiwa na umri wa miaka 18.

Baada ya muda mrefu kwenye Bundesliga, beki huyo alisajiliwa na Roma mwaka 2015 na kucheza ligi ya Serie A hadi 2017, alipojiunga na Ligi ya England baada ya kuhamia Chelsea.

Nguzo muhimu katika safu ya ulinzi ya Real Madrid, Antonio Rüdiger amejiimarisha tangu alipowasili katika klabu hiyo ya Hispania majira ya joto mwaka 2022.

Rüdiger ni mchezaji muhimu katika timu ya taifa ya Ujerumani na alicheza kwa mara ya kwanza mwaka 2014, ameicheza mechi 68. Ametoka kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara ya pili (baada ya taji la kwanza akiwa na Chelsea 2021).

### Nathan Ake (Uholanzi - Ivory Coast)

Ni beki wa kati, amecheza mechi 13 akiwa na kikosi cha kwanza cha Uholanzi. Pia ni beki wa klabu ya Manchester City.

Shirikisho la soka la Ivory Coast na kocha wa zamani wa timu hiyo, Marc Wilmots, walijaribu kumshawishi ajiunge na Ivory Coast mwaka 2017.

Lakini mchezaji huyo ambaye alikuwa akichezea klabu ya Bournemouth wakati huo, alikataa.

### Manuel Akanji (Sweden - Nigeria)

Alizaliwa Julai 19, 1995 huko Neftenbach, Sweden na baba Mnigeria, Manuel Akanji, alicheza mechi yake ya kwanza na Sweden, dhidi ya Visiwa vya Faroe Juni 9, 2017.

Amepitia Borussia Dortmund, Akanji alisajiliwa na mabingwa wa England Manchester City katika msimu wa 2022.

Wakati wa msimu 2022-2023, alitwaa ubingwa wa England, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya

### Jules Koundé (Ufaransa – Benin)

Amezaliwa kwa mama wa Ufaransa na baba wa Benin, Jules Koundé ni beki hodari katika ligi ya Hispania tangu 2019, alicheza Sevilla FC kisha Barcelona tangu Juni 2022.

Akiwa na umri wa miaka 25, mchezaji huyo ambaye bado ana familia nchini Benin, ameitwa katika timu ya Ufaransa tangu 2021. Wakati wa Kombe la Dunia la 2022, Jules Koundé alicheza kama mlinzi wa kati, alianza mashindano kwenye benchi, kabla ya kuchukua nafasi kama beki wa kulia.

Ni nafasi ambayo anaichezea klabu yake ya Barcelona.

### N'Golo Kanté (Ufaransa - Mali)

N'Golo Kanté anasifika kwa ustahimilivu wake, uwezo wake wa kurejesha mipira, unyenyekevu wake na ari yake.

Mali ni nchi ya wazazi wake. Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa aliitwa kwa mara ya kwanza na timu ya Ufaransa Machi 17, 2016.

Kanté alicheza mechi yake ya kwanza ya kulipwa katika Uwanja wa Stade Malherbe mjini Caen, kabla ya kung'ara kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na Leicester City kisha Chelsea.

Juni 2023 Mfaransa huyo aliondoka Chelsea baada ya miaka 7 katika klabu hiyo na kujiunga na klabu ya Saudi ya Al-Ittihad.



LEROY SANE

Kwa mara ya kwanza tangu aondoke Chelsea katika msimu wa mjira ya joto wa 2023 na uhamisho wake kwenda Saudi Arabia, N'Golo Kanté, anayechezea klabu ya Al-Ittihad, ameitwa kwenye timu ya Ufaransa kucheza Euro 2024, kwa sasa ana miaka 33.

### Denis Zakaria (Sweden - Sudan Kusini/Congo)

Denis Zakaria mwenye miaka 26, alizaliwa huko Geneva na mama kutoka Sudan Kusini na baba wa Congo.

Angeweza kuchezea moja ya nchi hizi mbili, lakini chaguo lake likawa Sweden, nchi yake ya kuzaliwa.Akiwa na umri wa miaka 17 tu, alicheza mechi yake ya kwanza Novemba 2014, dhidi ya FC Lausanne-Sport.

Kwa uwezo wake mkubwa, mwaka uliofuata 2015, alisajiliwa na Bern.

Katika msimu wa majira ya joto wa 2017, akiwa na umri wa miaka 21, Denis Zakaria aliondoka nchi yake ya asili na kujiunga na Bundesliga na Borussia Mönchengladbach.

Baada ya miaka mitano kukaa Ujerumani, alijiunga na Juventus Turin wakati wa dirisha la msimu wa baridi wa 2022 katika ligi ya Serie A na kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kisha alitolewa kwa mkopo kwenda Chelsea (alikocheza mechi 11, bao 1) wakati wa msimu wa 2022-2023, kisha akasaini mkataba wa misimu mitano Agosti 2023 na AS Monaco.

Aliwakilisha nchi yake katika mashindano makubwa manne ya mwisho ya kimataifa (Mashindano ya Ulaya ya 2016 na 2020 na Kombe la Dunia la 2018 na 2022).

Denis Zakaria, daima amethibitisha kushikamana na ukoo wake wa Kiafrika, husafiri hadi DRC kwenda kijiji cha mama yake, na huko Sudan Kusini, na huzungumza lugha zake za asili.

### Leroy Sane (Ujerumani - Senegal)

Mtoto wa mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Senegal Souleymane Sané. Mwanawe Leroy Sané ameamua kuichezea Ujerumani mwaka 2015.

Winga wa Bayern Munich, alikuwa kwenye vitabu vya Shirikisho la Soka la Senegal, angeweza kufuata nyayo za baba yake na kutetea rangi za Simba wa Teranga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, jina lake la kwanza ni heshima kwa Claude Le Roy, kocha wa zamani wa Senegal.

Leroy Sané, hajacheza mechi na timu ya Ujerumani tangu Novemba 2023, alitangaza kuwa yuko tayari kuichezea Ujerumani.

Jumatatu Juni 3, Wajerumani walitoka sare na Ukraine. Leroy Sané hakucheza kwani alikuwa bado anatumikia adhabu ya kutocheza mechi tatu.

Mechi dhidi ya Ugiriki mjini Mönchengladbach ni mazoezi ya mwisho ya Ujerumani kabla ya mechi yao ya kwanza ya Euro dhidi ya Scotland Juni 14. Winga wa Bayern Munich aliyewahi kuichezea Manchester City. Kocha wa Ujerumani Julian Nagelsmann alimwita Sané katika kikosi chake.

### Bukayo Saka (Nigeria – England)

Amezaliwa katika vitongoji vya London na wazazi wa Nigeria na aliwahi kuombwa na Shirikisho la Soka la Nigeria kujiunga na Super Eagles, winga huyo wa Arsenal anajiandaa kushiriki michuano ya Ulaya kwa mara ya pili.

Ni mchezaji wa kimataifa wa England tangu Oktoba 2020, Bukayo Saka alicheza mechi yake ya kwanza katika timu ya taifa ya England Novemba 2020.

Bukayo Saka anasema kuzaliwa na kukulia nchini Uingereza kulimzuia kuchagua timu ya taifa ya Nigeria. Alisema, ingekuwa vigumu kuchagua Nigeria kutokana na mazingira yake binafsi aliyokulia.

"Familia yangu yote imekuwa ikiishi Uingereza siku zote, itakuwa ngumu sana kwangu kuzoea mazingira ambayo sijawahi kuyapitia tangu utoto wangu," alisema.

Ameichezea England katika timu za vijana ya chini ya umri wa 16, 17, 18, 19 na 21.

Mshambuliaji huyo alishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Uingereza 2022 na 2023.

### Romelu Lukaku (Ubelgiji – DRC)

Romelu Lukaku alizaliwa Mei 13, 1993 huko Antwerp, mji wa bandari nchini Ubelgiji, na wazazi wa Ubelgiji-Congo.

Alianza kucheza kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miaka 16 akiwa na klabu yake ya mazoezi ya Anderlecht, ambayo ilimfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu hiyo ya Ubelgiji. Katika msimu wake wa pili wa kulipwa, 2009-2010, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alimaliza mfungaji bora katika ligi ya Ubelgiji.

Mwaka 2011, alijiunga na Ligi ya England kwa kusajiliwa na Chelsea lakini baadaye akatolewa kwa mkopo Kwenda West Bromwich na kufunga mabao 17 katika mechi 35 za ligi.

Lukaku aliendelea na maisha yake Uingereza kwa kucheza Everton kisha miaka miwili kucheza Manchester United.

Mwaka 2021, aliondoka Uingereza na kujiunga na ligi ya Serie A ya Italia akichezea Inter Milan ambapo alijaza mabao na kushinda taji na Nerra Zurri. Sasa ni mchezaji wa AS Roma, Romelu Lukaku yuko katika nafasi ya juu ya wafungaji katika wa timu ya taifa ya Ubelgiji.

### Kylian Mbappé (Ufaransa – Cameroon)

Kylian Mbappé alizaliwa na baba wa Cameroon na mama wa Algeria.

Bila shaka ni mmoja wa nyota wa michuano hii ya Ulaya 2024. Mbappé amesajiliwa na Real Madrid hivi karibuni, siku chache kabla ya kuanza kwa Euro 2024.

Alizaliwa na baba kutoka Cameroon na mama wa Algeria na alifanya chaguo la kuvaa jezi ya Ufaransa 2017 akiwa na umri wa miaka 18. Akiwa na umri wa miaka 25, baada ya misimu saba huko Paris Saint-Germain, tayari amepata mafanikio ya ajabu.

Mfungaji bora wa michuano ya kombe la dunia nchini Qatar 2022, amepata mataji kadhaa akichezea ligi ya Ligue 1, Mbappé tayari ana rekodi kubwa katika soka.

Alipoulizwa kuhusu ugumu wa kutwaa ubingwa wa Ulaya, mchezaji huyo mpya wa Real Madrid alisema, ni vigumu zaidi kushinda kombe la mataifa ya Ulaya kuliko Kombe la Dunia.


Akiteuliwa kuwa nahodha baada ya Kombe la Dunia la 2022. Atawaongoza wachezaji wenzake kwenye kombe la Ulaya, akiwa katika maisha yake ya ujana.

## Nukuu

"Tunaenda kwenye mashindano makubwa, hatuwezi kumuachia kila kitu Jude Belligham ingawa ni mchezaji mzuri na tunamtegemea,hapaswi kubebeshwa mzigo mkubwa" **Gareth Southgate Kocha wa timu ya taifa ya England.**



"Nina kila sababu na furaha ya kuendelea kubaki Manchester City kwa muda zaidi, nina furaha hapa na uchu wa mafanikio zaidi". **Golikipa wa Manchester City, Stefan Ortega akizungumzia maamuzi yake ya kusaini mkataba mpya ndani ya klabu hiyo.**



"Ni jambo la kujivunia kwangu na familia yangu, ni kitu ambacho unaweza kukiota ukiwa mdogo, ni kitu ambacho familia yangu wana furaha nacho," **Ethan Ampadu baada ya kuchaguliwa kuwa nahodha wa Wales kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Slovakia.**





Kikosi cha Yanga kilichotwaa Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

# KILICHOVUNWA NA KILA TIMU LIGI KUU 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

ULIKUWA ni msimu wa heka-heka, kwa timu 16 zilizochuana kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, na Kombe la Shirikisho.

**Baadaye timu zikaanza kujichuja, ipo iliyoonekana kuwa inataka ubingwa kwa maneno na vitendo uwanjani, zingine zilionekana kuupigania ubingwa kwa maneno tu, kuna zilizocheza ligi kimazoea, na zipo ambazo zenyewe zilikuwa zinasaka pointi za kuwawezesha kubaki Ligi kuu msimu ujao.**

Kuna zilizojikuta zikiwa kwenye mstari mwekundu, kila mechi zilipozidi kusonga mbele, pumba na mchele vilianza kujitenga.

Hadi kila timu ilipofikisha mechi ya 30, kila timu ilipata kile ilichostahili kuvuna katika nafasi iliyomaliza.

Mwandishi wa makala haya anachambua ushiriki wa kila timu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**1. Yanga**

Ilistahili kuwa bingwa, ilikuwa na kikosi imara chenye uwezo wa kupata ushindi uwanja wowote ule, nyumbani na ugenini. Ndiyo maana ilishinda mechi zote 15 ikicheza nyumbani.

Ilikuwa na wachezaji wenye uwezo, ubora, kasi, kujituma na kupambana kwa hali yoyote ile.

Imetwaa ubingwa kwa pointi 80 katika mechi 30, ikipoteza pointi 10 tu.

**2. Azam FC**

Imemaliza kwenye nafasi ya pili msimu huu ikicheza mechi 30 na kukusanya pointi 69, ambapo msimu ujao itacheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, Azam imepata nafasi ya pili kutokana na udhaifu wa kikosi cha Simba msimu huu.

Wingi wa mabao, na umakini katika mechi za mwisho baada ya mwenendo mbovu wa wapinzani wao waliokuwa wakitafuta nao nafasi ya pili, ukawebeba.

**3. Simba SC**

Umekuwa ni msimu mbovu kwa mara ya kwanza baada ya misimu sita. Mara ya mwisho Simba kushika nafasi ya tatu ilikuwa msimu wa 2015/16.

Haikuwa inavutia mashabiki wake uwanjani inapocheza licha ya kwamba ilikuwa inashinda mechi.

Ilionekana ina matatizo maeneo mengi, safu ya ushambuliaji, kiungo mkabaji, na mabeki wa pembeni.

Msimu huu inakwenda kucheza moja kwa moja Kombe la Shirikisho Barani Afrika, ikiwa na pointi 69, sawa na Azam, lakini ilizidiwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

**4. Coastal Union**

Ni mafanikio ya kwanza, baada ya miaka 26 tangu ilipotwaa Ubingwa wa Tanzania Bara mwaka 1988.

Msimu huu imemaliza nafasi ya nne, baada ya kuhangaika sana kubaki Ligi Kuu misimu michache iliyopita.

**5. KMC**

Kutoka kucheza 'play off' msimu uliopita dhidi ya Mbeya City, mpaka kumaliza nafasi ya tano yalikuwa ni mafanikio makubwa msimu huu kwa timu hiyo.

Na hayo yanaonekana kutokea mara baada ya kumpata kocha, Abdihamid Moalin, ambaye aliwahi kuifundisha Azam FC.

**6. Namungo FC**

Msimu uliopita ilishika nafasi ya tano, ikimaliza na pointi 40, lakini msimu huu imemaliza nafasi ya sita, ikikusanya pointi 36, nne pungufu ya 2022/23.

Ni timu ambayo inaonekana sasa inacheza Ligi Kuu kimazoea na haikuwa tishio kwa msimu hii miwili kama ilivyokuwa huko nyuma.

**7. Ihefu FC**

Pamoja na kuwa na wachezaji bora, wazoefu kutoka nchi mbalimbali, haikufikia ubora wa msimu uliopita, ilipomaliza nafasi ya sita ikiwa na pointi 39.

Msimu huu imeshuka nafasi moja chini, ikimaliza ya saba ikiwa na pointi 36, tatu pungufu ya za msimu uliopita.

**8. Mashujaa FC**

Mechi tatu za mwisho ndizo zilizoiokoa Mashujaa kubaki Ligi Kuu, ilikuwa chini na hali ilikuwa mbaya.

Ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Prisons ugenini, mabao 3-2 dhidi ya Mtibwa Sugar na ushindi dhidi ya Dodoma Jiji wa mabao 3-0, uliwatoa sehemu ya hatari, na si tu kuwaweka sehemu salama, bali maeneo ya juu ndani ya 10 bora kwenye msimamo, ikiwa na pointi 35.

**9. Prisons**

Haikuwa kwenye wakati mzuri mzunguko wa kwanza, lakini usajili wa dirisha dogo na mabadiliko madogo ya benchi la ufundi, kumleta kocha Ahmadi Ally, yaliibadilisha timu hiyo na kufanikiwa kumaliza katika nafasi ya tisa ikikusanya pointi 34.

**10. Kagera Sugar**

Imemaliza nafasi ya 10 ikwa pointi 34, lakini haikuwa kipya kwenye Ligi Kuu msimu huu. Ni moja kati ya timu iliyoendelea kucheza Ligi kuu kwa mazoea.

**11. Singida Big Stars**

Nafasi iliyomaliza ikiwa na pointi 33, iliathiliwa zaidi na baadhi ya wachezaji wake muhimu kuhamishwa na kupelekwa Ihefu FC. Baada ya hapo ikatoka kuwa timu ngumu na kuwa ya kawaida tu.

**12. Dodoma Jiji**

Ni timu ambayo tangu ilipopanda Ligi Kuu, haionekani kuwa na malengo zaidi ya kucheza tu ligi ili ibakie.

Imemaliza msimu ikiwa nafasi ya 12, na pointi zake 33, ikiponyoka kidogo katika mechi za mwisho kushuka daraja, au kwenda 'play off.'

**13. JKT Tanzania**

Ina bahati imesalia Ligi Kuu baada ya kushinda mechi yake ya mchujo dhidi ya Tabora United mabao 4-0, ikishinda ugenini na kulazimisha suluhu nyumbani.

Timu hii iliyopanda Ligi Kuu na kucheza kwa mara ya kwanza tangu ilipokuwa ikiitwa JKT Ruvu, ilionekana kukumbuka shuka kumekucha, lakini wamefanikiwa kubaki Ligi Kuu.

**14. Tabora United**

Inasubiri hatma yake kubaki Ligi Kuu kwenye 'play off' nyingine dhidi ya Biashara United, itakayoanza kupigwa Jumatano kwenye Uwanja wa Karume, Musoma, mkoani Mara.

**15. Geita Gold**

Haikuwa kwenye ubora wake wa misimu kadhaa nyuma, Msimu huu ilionekana kupata ushindi wake kwa kubahatisha.

Licha ya kwanza ilionekana hairuhusu sana mabao, lakini haikuwa na uwezo wa kufunga pia.

**16. Mtibwa Sugar**

Nadhani ilistahili kushuka daraja, kwani ilikuwa ikicheza ligi kimazoea.

Kwa misimu kama minne hivi, timu hiyo ilikuwa ikinusurika kushuka, kwa bahati nzuri mechi za mwisho zilimuokoa, au 'play off.'

**JE, WAJUA?**

SIMBA 1936 SPORTS CLUB

KLABU ya Simba kwa mara ya kwanza baada ya misimu sita imeshindwa kufuzu kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, msimu ujao itashiriki Kombe la Shirikisho baada ya kumaliza kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024.



# DRC, Tanzania zasaini mkataba kupewa hekta 60 kujenga bandari

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania na DRC zimesaini mkataba wa kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza manufaa ya kijiografia na ushindani kwenye shoroba kwa ujumla.

Mkataba huo ni kwa DRC kuipatia Tanzania eneo la hekta 60 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Kavu nchini humo kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mkataba huo ulisainiwa na Naibu Waziri Wa Uchukuzi Tanzania, David Kihenzile na Waziri anayeshughulikia masuala ya usafirishaji DRC, Marc Likombo, na kushuhudiwa na makatibu wakuu wa wizara hizo huku nchi ikiwakilishwa na Prof. Godius Kahyarara na Balozi wa Tanzania DRC, Said Mshana.

Akizungumza mara baada ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Profesa Godius Kahyarara alisema hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa itawezesha Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kutoa huduma ndani ya DRC na kuondoa ulazima wa wateja kuja mara kwa mara bandarini.

Alisema madereva wanaopeleka shehena DRC wataondokana na adha ya kusubiri kwa muda mrefu kwani mzigo ukifikishwa bandari kavu watakuwa na sehemu ya kukamilisha taratibu tofauti na hivi sasa ambapo kumekuwapo misongamano mingi barabarani wakisubiri ukamilishai wa nyaraka.

Aidha, alisema sekta binafsi nchini yakiwemo mabenki, wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali watakuwa na fursa ya kufungua biashara zao katika bandari kavu hizi ikiwamo masoko maalum.

Alisema bandari kavu hizo zitajengwa katika majimbo ya Katanga na Tanganyika.

Kwa mujibu wa Profesa Kahyarara, DRC inaagiza zaidi ya asilimia 80 ya vyakula pamoja na asilimia 90 ya bidhaa za viwanda ikiwemo vifaa vya ujenzi kama saruji, nondo nakadhalika.

"Ninaona hii ni fursa kubwa ya kukuza uchumi wetu, uwepo wa Bandari Kavu utaongeza uhakika wa upatikanaji wa mzigo wa kutosha kupitia bandari ya Dar-es Salaam,"alisema.

Aidha, alisema baada ya Bandari Kavu serikali kwa kushirikiana na ushoroba wa kati inaandaa mpango kabambe wa uwekezaji katika Ziwa Tanganyika kuwezesha Dar es Salaam kubaki kama lango kuu la nchi za ushoroba wa kati. Akizungumza mara baada ya kusaini mkataba huo, Naibu Waziri Wa Uchukuzi Tanzania, David Kihenzile alisema serikali imetenga jumla ya hekta 60 ambapo, hekta 15 za ardhi zimetengwa katika eneo la Bandari Kavu ya Katosho - Kigoma na hekta 45 katika eneo la Kwala- Pwani sambamba na kutoa hati miliki kwa ajili ya nchi ya DRC kujenga na kuendesha Bandari Kavu. Naibu Waziri Kihenzile alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha usafirishaji na uchukuzi unarahisishwa husani kwa mzigo mkubwa unaosafirishwa na DRC kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa DRC, Likombo alisema kwa DRC imetenga hekta 15 katika eneo la Kasumbalesa na hekta 20 katika eneo la Kasenga-Jimbo la Haut Katanga; na hekta 25 katika eneo la Kasambondo- Kalemie Jimbo la Tanganyika sambamba na kutoa hati miliki kwa ajili ya Tanzania kujenga na kuendesha bandari kavu.

Waziri Likombo aliongeza kuwa serikali ya DRC imefanya hivyo ili kurahisishwa biashara baina ya nchi hizo mbili kwani DRC inaitegemea sana Nchi ya Tanzania katika kusafirisha mizigo yake.

Mkataba huo unatajiwa kuongeza ufanisi na idadi ya mzigo unaosafirishwa katika myororo mzima wa uchukuzi, na kwamba takwimu zinazonyesha kwa 2022/23 tani milioni 3.5 za mzigo wa Kongo zilihudumiwa katika Bandari ya DRC.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akizungumza juzi na wananchi wa Manispaa ya Singida katika mfululizo wa ziara yake ya kutembelea majimbo yote ya uchaguzi ya mkoa wa Singida. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mwenyekiti UWT Singida aonya wazazi wasiopeleka watoto shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida , Martha Kayaga, amewaonya wazazi wasiopeleka watoto wao shuleni licha ya serikali kujenga shule nyingi na zenye ubora, huku akizitaka mamlaka kuchukua hatua kali za kisheria.

Akizungumza jana na viongozi na wananchi wa wilaya ya Iramba katika mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea wilaya zote za Mkoa wa Singida, alisema viongozi wa CCM wawe mstari wa mbele kuchukua hatua wanapoona kuna mzazi ambaye hajampelela mtoto wake kwenda shule.

"Shule zilizojengwa na serikali zina ubora na viwango vya juu kwa hiyo mzazi unampompeleka mtoto wako kwenye shule za gharama kubwa hiyo inakuwa ni anasa tu," alisema.

Kayaga alisema hivi sasa vitendo vya ukatili kwa watoto nyumbani vimekithiri ambapo watoto wanalawitiwa na kubakwa hivyo ni jukumu la kila mwananchi kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi au kwa viongozi wa kata na vijiji ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wahusika.

"Kinamama pazeni sauti haina maana Rais Samia anajenga shule halafu watoto wanashindwa kwenda shule kwasababu ya kufanyiwa ukatili, awe mume wako au ndugu akifanya vitendo vya ukatili mpelekeni polisi," alisema.

Kayaga akizungumza kuhusu mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri,alisema rais ameruhusu ianze kutolewa kuanzia Julai Mosi mwaka huu hivyo wanawake wakae tayari kwenda kukopa fedha hizo ili waweze kuanzisha biashara zozote ambazo zitawainua kiuchumi.

Aidha, aliwaomba madiwani kufuatilia vikundi vilivyokopeshwa kuhakikisha wanarejesha mikopo walivyokopeshwa ili na wengine waweze kukopeshwa.

Mwakilishi wa jumuiya hiyo taifa akitokea Mkoa wa Singida, Grace Mkoma aliwataka na kuwahamasisha wanawake wajasiriamali kuunda na kusajili vikundi, ili waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na Serikali kwa lengo la kuinua vipato vya wananchi.

# Naibu Spika atoa neno umuhimu bajeti jumuishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Spika Azzan Zungu amesema ili kwenda sambamba na utekelezaji wa dhana ya kuwa na bajeti yenye mlengo wa kijinsia, ni lazima kutazama kanuni za bunge kama zinakidhi ipasavyo kutekeleza dhana hiyo.

Aidha, amesema kama kanuni hizo zitakuwa na kasoro ziboreshwe ili kuwawezesha wabunge kushauri kuhusu bajeti kuzingatia masuala ya jinsia kwa minajili ya ustawi wa Taifa.

Aliyasema hayo juzi bungeni kwenye ukumbi wa Msekwa wakati akifungua semina iliyoandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Mashirika ya UN Women na UNDP kwa lengo la kuwaelimisha wabunge juu ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 na masuala ya Bajeti yanayozingatia Jinsia.

Zungu alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha bajeti ya serikali na taasisi zake zinazingatia masuala ya jinsia ikiwemo kushirikisha wadau katika uandaaji na utekelezaji wake.

Aidha, alizitaja jitihada nyingine ni kutenga mikopo ya wanawake na makundi maalum katika bajeti za halmashauri hapa nchini, ili kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika kujiletea maendeleo yao pamoja na ya taifa kwa ujumla.

"Naomba nichukue fursa hii pia, kuipongeza serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwa mstari wa mbele katika kufanikisha dhana hii ya bajeti inayozingatia jinsia," alisema Zungu.

"Naomba nitoe rai kwa wabunge kuzingatia semina hii ili tuweze kupata maarifa waliyotuandalia na hatimaye kutusaidia kujadili na kupitisha bajeti zijazo kwa jicho la kijinsia. Hii itawezesha kufanikisha mkakati wa serikali yetu wa kuhakikisha rasilimali za umma tunazozigawa na kuzisimamia zinawanufaisha Watanzania wote," alisisitiza Zungu.

Akizungumza katika semina hiyo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima alisema wizara ilifanya mapitio ya iliyokuwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 kwa lengo la kuiboresha ili kukidhi na kuendana na mahitaji ya sasa ya jamii ya kukuza usawa wa kijinsia katika masuala kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Alisema kwa sasa ipo Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 iliyozinduliwa Machi 8, 2024 na wizara kwa kutambua umuhimu wa sera hiyo imeona ni muhimu kuwapitisha wabunge waweze kuilewa kwa kuwa wana mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa.

"Pamoja na sera tutaelimishwa pia kuhusu umuhimu wa uzingatiaji wa bajeti ya mrengo wa kijinsia ili katika utekelezaji wa majukumu yetu tuweze pia kuwa na jicho la kijinsia," alisema Dk. Gwajima

Akiwasilisha kwa wabunge kuhusu Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dk. Seif Shekelaghe alisema uwepo wa sera hiyo imetokana na baadhi ya mapungufu ya utekelezaji wa sera iliyopita hivyo kutoendana na wakati uliopo.



# Serikali Mbarali yaweka msimamo kutoza ushuru

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali mkoani Mbeya, imetangaza msimamo wake wa kuendelea kuwatoza wakulima ushuru wa mpunga wanaposafirisha mahali popote ndani ya wilaya hiyo.

Aidha ushuru huo utagusa hata kama ni chini ya tani moja ambayo sheria mama hairuhusu kuwatoza.

Pia imesema itaendelea kuwatoza wakulima hao ushuru hata kama wanasafirisha kutoka shambani kwenda kuhifadhi nyumbani ama ghalani kwa maelezo kuwa isipotoza wakati huo kuna uwezekano wa mapato ya zao hilo kupotea.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila alitangaza msimamo huo mwishoni mwa wiki alipozungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa Kata za Kongoro Mswiswi na Miyombweni, na kwamba ushuru huo ni muhimu kwa maendeleo ya halmashauri hiyo, mkoa na Taifa.

Aliwataka wakulima hao kuchukua risiti na kuzihifadhi kila wanapotozwa ushuru huo, ili kuepuka kutozwa zaidi ya mara moja na kwamba kutokana na maendeleo ya teknolojia wananchi hao wanatakiwa kutunza hata namba za risiti ama kuzidurufu.

Kanali Mwila alisema katika wilaya hiyo asilimia kubwa ya wakulima wanalima kilimo biashara hali, ambayo inailazimu halmashauri hiyo kuwatoza ushuru hata kama wanatoa mpunga wao shambani kwenda nyumbani.

Alisema kwa sasa vijiji vingi vina maghala ya kuhifadhia mpunga huo na mashine za kukoboa na hivyo endapo hawatakuwa wanawatoza kuna uwezekano wa ushuru huo kupotea wakati wa mauziano kati ya wakulima na wafanyabiashara.

"Ushuru ni lazima wote tulipe, hata mimi mwenyewe mwaka huu nimeona nisiwe nasimuliwa tu, nimelima ekari 30 ambazo tayari nimeanza kuvuna na ninalipa ushuru kama kawaida, ushuru huu ni kwa ajili ya maendeleo yetu wenyewe," alisema Kanali Mwila.

Alisema wilaya hiyo kwa mwaka huu imepatiwa zaidi ya Sh. bilioni 170 na serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo zikiwemo Sh. bilioni 70 kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Alisema fedha hizo zinatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo ushuru wa mazo yanayozalishwa kwenye mikoa mingine na hivyo wananchi wa Mbarali lazima na wao washiriki kuchangia ushuru huo.

Diwani wa Kata ya Kongoro Mswiswi, Elia Leonard maarufu kwa jina la 'Bange' aliiomba serikali kuwaondolea wakulima ushuru uo kwa maelezo kuwa unawaumiza na ni kinyume na sheria mama ambayo hairuhusu kuwatoza wakulimana badala yake inaruhusu kuwatoza wanunuzi.

Alisema wakulima wamekuwa wakizuiwa njiani wanapotoka kuvuna mpunga na kutozwa ushuru huo huku akidai kuwa baadhi ya wakulima vyombo vyao vya usafiri vimekuwa vikikamatwa na kushikiliwa kwa sababu ya ushuru huo.

Alisema wakulima wamekuwa wakiumia kutokana na ushuru huo kutokana na gharama za uzalishaji kuwa kubwa, lakini bado wanatakiwa kulipa ushuru bila kuzingatia sheria mama ya ushuru.

"Tunaomba sana tuwapunguzie wakulima wetu mzigo huu wa ushuru, wanateseka sana maana wanatozwa wakiwa hawajafanya biashara yoyote, sasa mtu anaposafirisha mpunga kutoka shambani kwenda nyumbani anakuwa amepata wapi fedha?," alihoji Bange. Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kutunza amani na utulivu wakati serikali ikitafuta ufumbuzi wa tatizo la ushuru ambalo linaikabili wilaya hiyo.

Alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wakiwavamia maofisa wanaokusanya ushuru pamoja na magari ya polisi hali ambay inahatarisha amani na hivyo akawataka kuacha tabia hiyo.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi maarufu 'Sugu' (katikati) akishiriki kwenye mdahalo wa wazi wa mabadiliko ya katiba jijini Mbeya ulioandaliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS). **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## Mbaroni kwa kujeruhi wakigombea ardhi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia Mkazi wa Mtaa wa Kikula mjini Makambako, Martin Mgeni maarufu kwa jina la Lodilofa kwa tuhuma za kumjeruhi kwa kutumia mianzi na jiwe, Ronjinus Kusaga (61) kwa kile kilichoelezwa ni mgogoro wa ardhi.

Aidha majeruhi huyo amelazwa hospitali ya Inuka wilayani Wanging'ombe mkoani hapa kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza na Nipashe Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo na kueleza wanasubiri majeruhi huyo atoke hospitalini ili mtuhumiwa afikishwe mahakamani.

"Ni kweli mtuhumiwa tumemkamata lakini kwa sasa tunachosubiri ni yule majeruhi atoke hospitali alafu taratibu nyingine zitaendelea ikiwemo kumfikisha mahakamani," alisema Kamanda Banga.

Aidha, Kamanda Banga aliwataka wananchi kuzingatia ushauri unaotolewa na mabaraza ya ardhi na kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi. "Natoa rai kwa jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa sababu inaweza kusababisha madhara makubwa kwa jamii ikiwemo kifo," alisema Kamanda Banga. Awali, akizungumza kuhusiana na tukio hilo, Ronjinus Kusaga ambaye pia ni mkazi wa mtaa wa kikula ambaye ameshambuliwa alidai kuwa sababu ni mgogoro wa ardhi baina yao. "Martin Mgeni alivamia eneo letu na kuanza kulilima na wakati tunamfuatilia na kumuliza kwa nini amevamia eneo hilo ndipo akaanza kunishambulia," alisema Kusaga.

Kusaga alisema wakati tukio hilo linatokea mtuhumiwa Mgeni alikuwa na vijana wengine wawili na mara baada ya kutekeleza tukio hilo walimbeba na kwenda kumtupa msituni na kufafanua kuwa eneo ambalo lilivamiwa lina ukubwa wa zaidi robo ekari.

# Serikali yaleta mwarobaini kudhibiti ajali eneo korofi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeliagiza jeshi la Polisi kuandaa utaratibu wa malori na magari ya abiria kupita kwa awamu katika eneo la Mbembela, jijini Mbeya ili kuepusha uwezekano wa ajali kutokea.

Uamuzi huo umekuja siku chache baada ya kutokea ajali ya lori lililokuwa limebeba shehena ya kokoto kuvigonga vyombo vingine vya usafiri na kusababisha vifo vya watu 15 na majeruhi 16.

Aidha imemwagiza mkandarasi kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nne kusitisha kwanza maeneo mengine na kuanza ujenzi katika eneo hilo, ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea kwenye eneo hilo ambalo lina mteremko mkali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo alipowatembelea baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambapo alisema kwa sasa eneo hilo ndilo lililobaki kuwa korofi.

Alisema ndani ya miezi sita zimetokea ajali zaidi ya tatu ambazo baadhi yake zimegharimu maisha ya wananchi na hivyo akataka Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuandaa utaratibu wa magari kupita kwa awamu.

Vilevile aliwataka viongozi wa dini na wa mila wa mkoa huo kufanya maombi maalumu katika eneo hilo, ili kuzuia ajali ambazo zimekithiri kwenye mteremko huo. Kwa mujibu wa Homera, awali ajali nyingi zilikuwa zinatokea katika eneo la Mteremko wa Shamwengo na Mteremko wa Mlima Iwambi, lakini zikakoma baada ya kuwekwa utaratibu wa malori na magari ya abiria kupita kwa awamu.

"Naagiza TANROADS kuandaa eneo la malori na magari haya ya abiria kusubiriana kama ambavyo tulifanya Shamwengo na Mbalizi, lakini pia Mkandarasi anayejenga barabara yetu ya njia nne mwambieni afanye tathimini ili aanzie ujenzi hapa kabla ya maeneo mengine," alisema Homera.

Vilevile alilitaka Jeshi la Polisi kushirikiana na wadau wengine wa usafirishaji kutafuta njia mbadala ambayo itakuwa inatumiwa na pikipiki za magurudumu matatu maarufu 'bajaji' , ili kupunguza msongamano wa vyombo hivyo katika eneo hilo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Benjamin Kuzaga aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani, ikiwa ni pamoja na kuvikagua vyombo vyao kabla ya kuanza safari ili kuepusha ajali.

Alisema kwenye maeneo yote ya vizuizi wameweka maofisa wakaguzi wa magari, ili kujiridhisha kama magari hayo yanakuwa imara hasa kwenye mifumo ya breki na magurudumu.

Aidha, aliwataka wamiliki wa magari na madereva kusaidiana kuyakarabati magari yao, kuepusa ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara wa mara na kugharimu maisha ya wananchi.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji alisema siku ilipotokea ajali hiyo walipokea zaidi ya watu 30 ambao baadhi walifikishwa hospitalini hapo wakiwa tayari wameshafariki.





## Miundombinu ya elimu kuendelea kuimarishwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein amesema serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya elimu, ikiwemo ujenzi wa maabara ili kuwapa fursa wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki wakati wa hafla fupi ya kukabidhi kompyuta mpakato wasichana 50 walioshiriki kwenye mpango wa umoja wa mataifa kwa wanawake wa Afrika (Binti kidijitali) iliyohusisha mafunzo ya kidijitali kwa wanafunzi wa kike.

Alisema kabla ya wanafunzi kujiunga na elimu ya juu kuna haja ya kuandaliwa vyema na kupatiwa vifaa vya kujifunzia, ili kupata uelewa wa kutumia nyenzo za kujifunzia wakiwa katika umri mdogo.

Waziri Hussein alisema pia serikali imekuwa na utaratibu wa kuwapa kompyuta mpakato (laptop) wanafunzi wanaofanya vizuri ili kuwasaidia katika harakati zao za masomo.

Alisema serikali ikichukua juhudi mbalimbali ili teknolojia kuanza kutumika katika ngazi ya msingi shuleni na mabadiliko ya elimu hasa katika miundombinu, na kwamba serikali imeboresha miundombinu hiyo na kumuwezesha mwanafunzi kutumia mifumo ya kidijitali.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao waliopatiwa kitendea kazi hicho cha komputa hizo kuwa mabalozi wazuri katika jamii na kuwasaidia wanafunzi wengine kuingia katika masuala ya kidijitali na kuacha kutumia mitandao kwa kufanya vitu ambavyo haviendani na maadili.

Mwakilishi Shirika la Umoja wa Mataifa linalotetea haki za Wanawake (UN Women), Peterson Magoola alisema makadirio ya hivi karibuni, asilimia 90 ya kazi zijazo ulimwenguni kote zitahitaji ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Hata hivyo, alisema ni wasichana wachache kuliko wavulana wanaoandikishwa katika masomo ya sayansi na wanawake wana nafasi ndogo katika taaluma za sayansi na uhandisi.

"Ikiwa waafrika, na kwa hakika, wanawake na wasichana wa Kitanzania na Wazanzibari watafanikiwa katika soko la ajira siku zijazo, wanahitaji ujuzi wa ICT, kuwapa ujuzi huu ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi ya bara hili na kwa fursa za wasichana binafsi katika soko la ajira la siku za usoni," alisema.

Alisema mkakati wa UN Women ndani ya kanda kupitia mpango wa African Girls Can Code Initiative (AGCCI), unalenga kuimarisha uwezo wa wanawake vijana kupitia kambi za usimbaji, kuingiza TEHAMA, kuweka misimbo na jinsia katika mitaala ya shule.

Aidha, aliwataka wasichana hao kubuni masuluhisho ya kushughulikia changamoto za kijamii zinazowakabili wanawake na wasichana, kama vile unyanyasaji wa kijinsia, upatikanaji wa elimu, na ukosefu wa usawa wa kiuchumi.

Mtaalamu wa uwezeshaji wanawake kiuchumi kutoka shirika hilo, Lilian Mwamdanga aliwashauri mabinti kutumia mitandao ya kijamii, ili iwape fursa za ajira na kujikwamua kiuchumi kwa kujiajiri na kuajiri wengine.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Shufaa Said alisema ujuzi wa kidijitali utasaidia kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuwafanya wasichana kuingia kwenye kazi za ubunifu kwa kutumia teknolojia hizo.

# Wizara, FAO wazindua kampeni ya lishe bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), imezindua kampeni ya lishe bora kwa njia ya daladala.

Lengo ni kuongeza uelewa kwa wanajamii wote, juu ya matumizi sahihi ya vyakula vinavyowazunguka na hivyo kuhamasisha ulaji unaofaa kwa kila mmoja.

Akizungumza jana katika uzinduzi huo uliofanyika katika Soko la Kibandamaiti visiwani humo, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis alisema kampeni hiyo itapunguza matatizo ya lishe miongoni mwa wazanzibari.

Pia itapunguza tatizo la utapiamlo kwa watoto pamoja na tatizo linaloongezeka kwa kasi la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo kisukari, shinikizo la damu na baadhi ya magonjwa ya saratani.

Alisema elimu hiyo muhimu itakayotolewa kwa njia ya usafiri wa daladala ni kwa mujibu wa mwongozo wa Taifa wa chakula na ulaji sahihi uliotolewa na wizara yake kwa kushirikiana na FAO na mwongozo huo umezingatia uwepo na matumizi ya vyakula vya asili vilivyopo na kuelekeza vipimo sahihi kwa kila mlo chakula au kinywaji ambacho binadamu anatakiwa kupata kwa siku.

"Wataalamu wa lishe wanaelekeza kwamba lishe bora haikamiliki kwa uwepo wa chakula kwa wingi tu, bali pia iambatane na uelewa juu ya matumizi sahihi ya chakula hicho kwa kuzingatia mahitaji ya mwili na rika,"alisema Shamata.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na vyakula vya kila aina hata hivyo watu wake wanakosa maarifa katika kupangilia vyakula hivyo kwa usahihi, ili kupata mlo kamili ikiwemo pia kuzingatia matumizi ya vyakula mchangayiko toka makundi sita ya vyakula kama inavyoelekezwa kwenye mwongozo wa kitaifa wa chakula na ulaji.

"Shukrani nyingi nazitoa kwa Umoja wa Ulaya (EU) kupitia mradi wa AgriConnect na FAO, kwa kuridhia kufadhili mchakato mzima wa mwongozo huu hata kuendelea kufadhili utoaji wa elimu kwa watanzania, ili kuongeza uelewa wa wananchi wetu juu ya ulaji unaofaa"alisema.

Mratibu wa FAO Zanzibar, Leila Miraji alisema usalama wa chakula ni jukumu la kila mtu na kwamba FAO na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) wana majukumu makuu katika kuweka viwango vya kimataifa vya chakula, ili kulinda afya za watumiaji na kuhakikisha mazoea mazuri katika biashara ya chakula. Aidha, alisema mtu mmoja kati ya kumi duniani hupata maradhi baada ya kula chakula kisicho salama kila mwaka na maradhi yanayosababishwa na chakula kisicho salama yanakadiriwa kusababisha vifo vya watu 420,000 kila mwaka. Alisema kati ya hao, vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano ni 143,000 na athari kwa watoto walio chini ya miaka mitano ni kubwa.

Mratibu huyo alisema usalama wa chakula unaweza kuathiriwa na matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu vya mazao na mifugo, utunzaji wa mazao ya mimea, mifugo na viumbe wa majini usio sahihi, sumu za viwandani na vihifadhi vya vyakula mbalimbali, vifungashio visivyo sahihi.

Aidha, alisema utapiamlo bado ni changamoto kutokana na kuongezeka kwa visa vya uzito na unene kupita kiasi miongoni mwa watoto na wanawake wa umri wa kuzaa katika maeneo ya vijijini na mijini Pia alisema kuna ushahidi wa ongezeko la mzigo wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayohusiana na lishe.

Leila alisema mojawapo ya mikakati bunifu ya kukabiliana na changamoto hizo, wanatumia usafiri wa umma wa mabasi madogo, yanayojulikana daladala, kuhamasisha umma juu ya mazoea mazuri ya lishe kwa kutumia mwongozo mpya wa chakula na ulaji. Alisema wanatarajia kufanya ziara za kielimu katika miji mikuu mitatu ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, na Zanzibar na kuwafikia takriban watu 9,000 moja kwa moja na watu milioni 10 kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa muda wa siku 30 kutoka Juni hadi Julai mwaka huu.




Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis (alievaa kofia) akizindua kampeni ya lishe bora kwa njia ya usafiri wa daladala hafla ambayo imefanyika jana katika Soko la Kibandamaiti mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tamasha laandaliwa kuvutia utalii, uwekezaji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeandaa tamasha la maonesho ya utalii na uwekezaji kwa ajili ya kuvutia na kutangaza fursa za uwekezaji wenye tija katika maeneo mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana visiwani humo kuhusu maonesho hayo, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga alisema uchumi wa Zanzibar umepitia mabadiliko makubwa na sekta ya utalii ikiendelea kushamiri kutokana na ongezeko la wageni.

Alisema idadi ya wageni walioingia Zanzibar mwaka jana 2023 imefikia 638,498 sawa na ongezeko la asilimia 16.4 ikilinganishwa na 548,503 walioingia mwaka 2022 na ina matarajio makubwa kuongezeka kwa wageni hasa kupitia uzinduzi wa safari za ndege mwishoni mwa Juni, Julai na Agosti ambapo miezi hiyo ni ya msimu mkubwa wa utalii.

Soraga alisema tamasha hilo litakuwa ni jukwaa la kimataifa la kuonesha Zanzibar utamaduni wake uliohai na uwezo wake mkubwa wa uwekezaji, kuvutia watalii, wawekezaji na wataalamu wa sekta kutoka Tanzania, Afrika na duniani kote.

Aidha, alisema maonesho hayo yatavutia na kutoa nafasi nzuri kwa wawekezaji na kutoa maarifa ya kina kuhusu soko la Zanzibar kupitia warsha na semina za kipekee zitakazokwenda sambamba na maonesho hayo.

"Washiriki watapata fursa ya kujionea maendeleo mapya ya soko, maeneo mapya na bidhaa mpya za kitalii ambazo zinaweza kuongeza thamani kubwa kwenye orodha zao za uwekezaji na kutoa uzoefu wakipekee kwa watalii na wageni.

Waziri huyo alisema Zanzibar ina fursa nyingi za uwekezaji kutokana na urithi wake wakipekee wa utamaduni wake mzuri wa asili.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Aboud Suleiman Jumbe alisema kuutangaza utalii kupitia maonesho hayo ni jambo jema hasa katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa wa utalii tangu kumalizika kwa ugonjwa wa Uviko 19.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii, Hafla Mbamba alisema wameamua kufanya tamasha hilo ili kuendelea kuwavutia watalii na kuitangaza Zanzibar kimataifa kupitia sekta ya utalii.

# ‘Wazalishaji vyakula vya mifugo wawasilishe sampuli zao TVLA’

**Na Halfan Chusi**

WAZALISHAJI vyakula vya mifugo nchini wametakiwa kuwasilisha sampuli za vyakula katika Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) ili kuhakikiwa ubora kabla ya kupelekwa sokoni.

Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk. Stella Bitanyi alielekeza hayo juzi jijini Dar es Salaam baada ya timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na TVLA kukamilisha ukaguzi wa viwanda vya vyakula na kufanya kikao cha utoaji mafunzo kwa wazalisha, wauzaji na watumiaji wa vyakula vya mifugo,

Dk. Bitanyi alisema wazalishaji hao wanapaswa kuwasilisha sampuli katika maabara za wakala ili wapatiwe ushauri wa vyakula hivyo, kwamba sheria inataka chakula kisicho bora kisingizwe sokoni ili kumlinda mfugaji.

“Wazalishaji vyakula vya mifugo wahakikishe wanaendelea kuzalisha vyakula bora ili wafugaji waweze kukinunua chakula hicho ili kupata matokeo mazuri kwa mifugo yao,” aliagiza Dk. Bitanyi.



Akiongoza timu ya ukaguzi, Mkurugenzi wa Huduma za Uchunguzi kutoka TVLA, Dk. Zacharia Makondo, alisema ni muhimu kwa vyakula vya mifugo kufika sokoni kama vilivyowekwa viwandani na kwamba wanaopuuza watachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama.

Dk. Makondo alisema kuwa katika ukaguzi wamegundua baadhi ya wauzaji vyakula vya mifugo wanachanganya vyakula wenyewe bila kufuata utaratibu.

Alisema ni makosa kwa wauzaji wa vyakula vya mifugo kuchanganya vyakula wenyewe na kuwauzia wafugaji.

Alisema pia ni makosa kwa wauzaji vyakula vya mifugo kufungua mifuko kutoka viwandani na kuchanganya na vyakula vingine.

Baadhi ya wadau walioshiriki katika ukaguzi walipongeza kuwapo ukaguzi wa vyakula vya mifugo, wakisema itasaidia kuhakikisha vinakuwa bora na kumnufaisha mfugaji ili apate matokeo mazuri ya mifugo yake.

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania unatarajia kuendelea kutoka elimu na kufanya ukaguzi wa rasilimali na vyakula vya mifugo katika kanda mbalimbali za wakala pamoja na kusimamia sheria ili wafugaji waweze kufuga kwa tija na kupata matokeo bora kupitia ufugaji.

# Neema tele kituo kipya cha ubunifu

**Na Salome Kitomari,** aliyekuwa KOREA

SERIKALI imesema imekubaliana na Korea kujenga chuo cha TEHAMA ambacho kitakuwa na kituo cha ubunifu katika eneo la Nala, jijini Dodoma.

Kituo hicho kitakusanya wabunifu bila kuangalia kiwango cha elimu yao kisha kuwaatamia kwa ajili ya kukuza vipaji, kampuni ndogo na kuongeza ajira.

Mwishoni mwa wiki, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alibainisha hayo alipotembelea kituo cha ubunifu cha Gyeoggi Center for Creative Economy &Innovation, jijini Seoul, Korea Kusini ikiwa ni sehemu ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha itatungwa sera itakayosaidia wabunifu wanaochipukia nchini, kwa kuwa ni lazima kuwa na mifumo ya kisheria ambayo huanzia kwenye sera, sheria kisha kanuni.

Kwa mujibu wa Waziri Nape, kuna changamto mbalimbali za kuendeleza ubunifu nchini; uwekezaji mkubwa utafanyika.

Alisema fedha za awali zilizotolewa ni Dola 600,0000 (Sh. bilioni 1.6) kwa ajili ya upembuzi yakinifu na ukikamilika, watapata fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo.

“Tunatarajia kuanza ujenzi wa kituo kitakachoatamia wabunifu, kupitia ziara hii tumekubaliana ili tuwekeze kwenye nguvukazi ya TEHAMA,” alisema Waziri Nape.

“Ubunifu hautathiminiwi kwa vyeti, unaweza kuwa bila vyeti, tunachotaka ni kuwa na kituo kitakachopokea vijana wa Kitanzania wabunifu hata kama ni darasa la saba, tutajenga vituo vinane nchini lakini hiki cha Dodoma kitakuwa kikubwa.

“Lengo ni kulea wabunifu bila kujali elimu, kuna watakaoingia kwa elimu yao na wengine kwa ubunifu wao. Dunia ya leo watu wengi waliobuni hawana elimu kubwa. Tunatamani tuwe na mfumo utakaowachukua bila kujali elimu yao,” alisema.

Waziri Nape alisema kwa maelekezo ya Rais Samia kitajengwa chuo cha TEHAMA ambacho ndani yake kutakuwa na kituo cha kusaidia ubunifu.

“Tunatamani kuwa na program kama hizi nyumbani, tuna vijana wengi sana wenye uwezo mkubwa wa kufanya ubunifu mbalimbali, ninaamini tukiwa na kituo kama hiki tutawasaidia Watanzania wengi, tutaongeza ajira na kuchangia ukuaji uchumi,” alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Startup Association, Zahoro Muhaji, alisema sekta hiyo inakua kwa kasi. Hivi sasa kuna zaidi ya wanachama 700 wanaofahamika, na sekta imevutia uwekezaji mkubwa wa mitaji kuingia katika uchumi wa nchi.

“Kwa miaka mitatu iliyopita tumevutia zaidi ya Dola milioni 200 (Sh. bilioni 500) zimeingia kama uwekezaji kwenye startups za Tanzania, changamoto kubwa inayotukabili ni mifumo ya kisera, sheria na kanuni kutokana na kwamba ni jambo jipya na mifumo haijaandaliwa kwa aina hiyo ya biashara.

“Nyingine ni mitaji ya fedha na ujuzi, yakitatuliwa yanaweza kutusogeza mbele, ndio maana tupo karibu na serikali ili kutengeneza sera ya startup nchini kwa sababu nchi nyingi za Afrika zimeshatengeneza hadi sheria za kuzisaidia.

“Lakini pia kuongeza ujuzi na mazingira mazuri ya startup kuongeza ujuzi wao. Tunaamini itasaidia kukuza na kuendeleza vijana,” alisema.

Korea imepiga hatua kubwa kimaendeleo baada ya mmoja wa marais wa nchi hiyo kuita kampuni 15 na kuzipa mtaji kisha kuwa na ufuatiliaji wa karibu, ikafanikiwa kuwa kampuni kubwa duniani, zikishikilia uchumi wa nchi hiyo kwa asilimia 80.


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 9621 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BASIL NICHOLAS ALEXANDER JENNINGS BRAMLY**
**ANNA ELISABETH JENNINGS BRAMLY.........MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 26 mwezi wa 06, 2024 saa 2:30 Asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji A.A Omari.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 20 mwezi wa Mei, 2024

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA CHETI NA TRANSCRIPT YA CHUO



**HIJA KASIMU** anatangaza kupotea kwa **TRANSCRIPT** na **CHETI CHA CHUO CHA KOZI YA PROJECT PLANNING AND MANAGEMENT** chenye usajili namba **IRDP/BDPPM/17/118** kilichotolewa na **INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING (IRDP)** mwaka **2020.**

Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/22258/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP 117 R.R. 2002)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

BY THIS DEED, I IRENE JOHN ABANA, a citizen of Tanzania and a resident of Dar es salaam, DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounces, relinquish and abandon the use of my former name of MARIAM ABDALLAH MAKANGE, and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of IRENE JOHN ABANA.

For the purpose of evidence of such determination, I HEREBY DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deeds, documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings transactions and creations whatsoever use and subscribe the name of IRENE JOHN ABANA as my name in lieu of and substitution for my former name of MARIAM ABDALLAH MAKANGE and the aforesaid changes are due to “Religious factors” as I have freely converted from Muslim to Christianity.

AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the name of IRENE JOHN ABANA.

IN WITNESS WHEREOF I, hereon substitute my old name MARIAM ABDALLAH MAKANGE , by new name of IRENE JOHN ABANA, I have set my hand at Dar es salaam.

SIGNED and DELIVERED by the Said IRENE JOHN ABANA Who is known to Me personally in my presence This 31st day of May, 2024 — Irene — DEPONENT

BEFORE ME:-
Name: FELIX JESSE
Signature:
Postal address: 75513 DSM
Qualification: ADVOCATE, COMMISSIONER FOR OATH & NOTARY PUBLIC



## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**LEILA MCHARO KUMBA** anatangaza kuotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 543445 iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/110252/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA GEITA**
**LILILOPO GEITA**
**MAOMBI NA 14/2024**
**MAGAMBO NKILOSUBI MAGAMBO ...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**

- **ZAKARIA ALEX**
- **KUDRA RAJABU**
- **KWITEGA MAGANGA..................WAJIBU MAOMBI**

**WITO**

Kwa KWITEGA MAGANGA popote ulipo unafahamishwa kwamba mleta maombi tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhidi yako katika Baraza la ardhi na Nyumba la wilaya Geita lililopo Geita, maombi haya yamepangwa tarehe 11/06/2024 kwaajili ya kutajwa /kusikilizwa.

Hivyo basi unaamriwa kufika shaurini katika ofisi za Baraza saa 3:00 Asubuhi wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote aliyeruhusiwa kisheria. Nakala ya madai inapatikana katika Ofisi za Baraza.

KAA UKIJUA kwamba kushindwa kufika kwako, Baraza litasikiliza shauri na kutoa hukumu/ maamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya baraza hili leo tarehe 28/05/2024

MASAO, E
MWENYEKITI
28/05/2024

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARY M. KITAMBI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI GRANDE yenye usajili namba T 683 BJG. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/1081-48/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IRINGA**
**SHAURI LA MASAHIHISHO YA ARDHI NA.03 YA MWAKA 2023**
**1.NATASHA DANSTAN MPANGALA.....................MWOMBAJI**
**2.TULIKISA JAQULINE GOODLUCK KIPPA@ TULIKISA JAQUILINE GOODLUCK KIPIGAPASI............................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1.ALIMONI SIMONI CHAULA under power of attorney of GOODLUCK LEONARD KIPIGAPASI.........MJIBU MAOMBI**
**2.ALICY LEONARD KIPIGAPASI..........MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**Kwa: ALICY LEONARD KIPIGAPASI**
**POPOTE ULIPO.**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa tarehe 18/06/2024 saa tatu kamili [9:00] asubuhi mbele ya Mhe.A.E. Mwipopo,Hivyo basi kama mjibu maombi namba mbili [2] katika shauri hilo unatakiwa kufika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa wewe mwenyeweama kupitia Wakili/Mwakilishi wako anayetambulika kisheria. Fahamu kuwa endapo kama autafika katika siku hiyo au kutuma Mwakilishi wako, shauri hilo litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo. Imeasainiwa hapa Iringa leo tarehe 24 mwezi April 2024.

**MALEWO M.A**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA IRINGA.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**RADHIA TOTO KASSY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0454-0048** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. JOSEPH NGARENARO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014, cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0673 – 0661 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NAGWA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2017** , **TRANSCRIPT NA CHETI CHA CHUO** chenye namba ya usajili IRDP/BDPPM/17/18 kilichotolewa na **INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING (IRDP)** mwaka **2020** na **CHETI CHA MASTERS DEGREE** *in* **PROJECT PLANNING MONITORING AND EVALUATION** chenye namba ya usajili **IRDP/MPPME/20/000062** kilichotolewa na **INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING (IRDP)** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/22250/2024**
**PHQ/DOD/DOD/22246/2024**

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yawaokoa mateka wanne Gaza

**JERUSALEM,** Israel

JESHI la Israel limewaokoa mateka wanne waliokuwa wanashikiliwa na Hamas tangu shambulio la Oktoba 7, katika operesheni kubwa zaidi ya kuwakomboa mateka tangu kuanza kwa vita na Hamas huko Ukanda wa Gaza.

Jukwaa linalowaunganisha ndugu na jamaa wa mateka wanaoshikiliwa na Hamas huko Gaza lilipongeza uokoaji wa mateka hao wanne kutoka kwenye ardhi ya Palestina juzi.

Jukwaa hilo lilisema operesheni ya kishujaa ya jeshi la Israel ambayo iliwezesha kuokolewa kwa Noa Argamani, Shlomi Ziv, Andrey Kozlov, na Almog Meir Jan ni ushindi wa kimiujiza.

**Tumejitolea kufanya hivyo katika siku zijazo pia. Tutafanya hivyo na hatutokata tamaa hadi tukamilishe azma yetu ya kuwarejesha nyumbani mateka wote ima wawe hai au wamekufa.**

"Pia tunaendeleza juhudi kwa jumuiya ya kimataifa ili kuhakikisha tunaishinikiza Hamas kuwaachilia mateka wengine," alisema.

Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu alisema kuwa Israel haitozuiliwa na ugaidi na kwamba itaendelea na operesheni yake kwa ubunifu na ushujaa ili kuwarejesha nyumbani mateka wote wanaoshikiliwa na Hamas huko Gaza.

"Tumejitolea kufanya hivyo katika siku zijazo pia. Tutafanya hivyo na hatutokata tamaa hadi tukamilishe azma yetu ya kuwarejesha nyumbani mateka wote ima wawe hai au wamekufa," alisisitiza Netanyahu.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz alisema taarifa ya kuokolewa mateka wanne wa Israel ni ishara yenye kuleta matumaini.

Kiongozi wa Kundi la Hamas Ismail Haniyeh alisema kamwe Israel haiwezi kuwalazimisha matakwa yao, huku akisisitiza kwamba hawatoafiki makubaliano yoyote ambayo hayatozingatia usalama kamili wa Wapalestina.

Haniyeh alitoa kauli hiyo kujibu tukio la hivi karibuni zaidi la jeshi la Israel kulishambulia eneo la al-Nuseirat katika Ukanda wa Gaza ambako hadi sasa inaarifiwa kuwa watu wasiopungua 55 waliuawa.

Aidha, Israel ilidai kuwa mateka wawili kati ya wanne waliookolewa walipatikana eneo hilo la al-Nuseirat.

Mamlaka za Hamas, ambayo imeorodheshwa na Umoja wa Ulaya, Marekani, Ujerumani na mataifa kadhaa ya Magharibi kama kundi la kigaidi zimesema idadi ya watu waliouawa katika shambulio la Israel huko Nuseirat imefikia 93.

Katika taarifa ya Haniyeh alisema "watu wetu kamwe hawatajisalimisha na wataendelea kupambana na kutetea haki zao dhidi ya adui huyu mhalifu. Ikiwa wavamizi wa Israel wanadhani kwamba wanaweza kutulazimisha matakwa yao kwa kutumia mabavu, basi wanajidanganya kabisa."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Israel imeendeleza mashambulizi yake huko Gaza na kujikita zaidi katika eneo la katikati mwa ukanda huo. Hayo yanajiri licha ya Israel kulaumiwa baada ya kuishambulia shule inayosimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA).

Vile vile, serikali mjini Tel-Aviv imekuwa ikikabiliwa na ukosoaji mkubwa kufuatia mashambulizi yake katika maeneo ya makazi ya raia, kambi za wakimbizi na shule.

Waziri wa Israel anayehusika na mikakati ya vita ametishia kujiuzulu baada ya kuongezeka kwa shinikizo kubwa kutokana na mwenendo wa nchi yake katika operesheni ya kijeshi huko Gaza ambayo hadi sasa kulingana na Wizara ya afya inayodhibitiwa na Hamas, tayari imesababisha vifo vya Wapalestina zaidi ya 36,000. **DW**

## Wanajeshi watano wauawa na Al Shabab Somalia

**MOGADISHU,** Somalia

SERIKALI nchini Somalia imesema wanajeshi watano wameuawa katika shambulizi lililotekelezwa na wanamgambo wenye itikadi kali wa Al Shabab katika eneo la kaskazini mwa mji Mkuu wa Mogadishu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na serikali, vikosi vya serikali, vikiungwa mkono na wanamgambo wa eneo hilo, vilikuwa na taarifa kuhusu shambulio lililopangwa katika wilaya ya Ceeldheer na Al Shabab, kundi lenye uhusiano na Al-Qaeda, na kutekeleza shambulio la kuvizia.

Ilielezwa kuwa kundi la Al Shabab, limekuwa likipigana na serikali ya shirikisho inayoungwa mkono na jumuiya ya kimataifa kwa zaidi ya miaka 15.

Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamoud alitangaza vita kamili dhidi ya wanamgambo hao Septemba 2023, huku akianzisha mashambulizi ya kijeshi, hasa yaliyosaidiwa na mashambulizi ya anga ya Marekani.

Licha ya hayo, inaelezwa kuwa Al Shabab wanaendelea kufanya mashambulizi ya umwagaji damu kwa kulipiza kisasi, wakionyesha uwezo wao wa kushambulia katikati ya miji ya Somalia na vituo vya kijeshi.

Ilibainishwa kuwa Mei 26, mwaka huu, walishambulia kambi iliyokuwa na wanajeshi wa Uganda wa kikosi cha Umoja wa Afrika nchini Somalia (ATMIS) kusini mwa nchi hiyo na kuua takriban wanajeshi 54.

Pia Oktoba 29, 2022, mabomu mawili yaliyotegwa ndani ya gari yalilipuka huko Mogadishu, na kuua watu 121 na wengine 333 kujeruhiwa. Ikielezwa kuwa lilikuwa shambulio baya zaidi kuwahi kutokea katika kipindi cha miaka mitano katika nchi hiyo. **RFI**



Wanaotuhumiwa kujaribu kumpindua rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wakiwa katika mahakama ya kijeshi katika mji mkuu wa Kinshasa. **PICHA: MTANDAO**

# Waliotaka kufanya mapinduzi DRC kortini

**KINSHASA,** DRC

KESI ya watu 51, wakiwemo Wamarekani watatu, wanaotuhumiwa kujaribu kumpindua Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwezi Mei mwaka huu, imeanza kusikilizwa katika mahakama kijeshi nchini humo.

Inaelezwa kuwa kesi hiyo inaonyeshwa moja kwa moja kwenye TV na redio ya taifa kutoka jela ya kijeshi ya N'dolo katika mji mkuu wa taifa hilo Kinshasa.

Washtakiwa hao walifikishwa katika mahakama ya kijeshi wakiwa wamevalia mashati ya bluu na manjano, ikiwa ni mara ya kwanza kuonekana hadharani tangu mapinduzi hayo kushindwa.

Waliokamatwa wakati wa mashambulizi kwenye ikulu ya rais na nyumba ya mshirika wa Rais Félix Tshisekedi, wanakabiliwa na mashtaka mengi, ikiwa ni pamoja na kufadhili ugaidi, mauaji na jaribio la mauaji.

Wizara ya mambo ya nje ya Marekani ilisema haijapewa fursa ya kuwafikia raia wake walioko kizuizini.

Watu sita waliuawa wakati wa jaribio la mapinduzi Mei 19, mwaka huu, akiwemo mshukiwa kiongozi wa njama hiyo Christian Malanga.

Washtakiwa wengine walizuiliwa baada ya mashambulizi dhidi ya Palais de la Nation na nyumba ya Vital Kamerhe, ambaye ni spika wa bunge.

Ripoti za vyombo vya habari vya ndani zilisema washambuliaji hao walikuwa wanachama wa Vuguvugu la New Zaire lenye uhusiano na Malanga, mwanasiasa wa zamani wa DRC ambaye alipata uraia wa Marekani.

Ilielezwa kuwa motto wa Marcel Malanga ni miongoni mwa raia wa Marekani waliokamatwa.

Mwingine ni Tyler Thompson mwenye umri wa miaka 21, ambaye familia yake iliiambia BBC kuwa hawakuwa na wazo lolote jinsi alivyojiingiza katika mpango huo.

Watu wengine wa mataifa tofauti pia walihusika na wako mahakamani, kwa mujibu wa msemaji wa jeshi Jenerali Sylvain Ekenge.

Mmoja ni raia wa Congo ambaye ana uraia wa Ubelgiji na pia kuna raia wa Canada mwenye asili ya DRC. **BBC**

# EATV YAZINDUA UPYA KIPINDI CHA '5 SELEKT'

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Runinga cha East Africa Television (EATV) jana kimezindua upya kipindi cha burudani kinachowalenga vijana cha 5 Selekt kikiambatana na matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumtangaza mtangazaji mpya wa kipindi hicho.

Mbali na kumtambulisha mtangazaji mpya, wamezindua vipengele na muonekano mpya utakaoanza kuonekana sasa.

Kipindi hicho chenye ushawishi mkubwa kwa vijana kinachorushwa kila Jumatatu hadi Ijumaa saa 11:00 jioni, kimemrudisha mtangazaji maarufu, Tonny Albert 'Tbway 360' aliyekuwa mapumziko kwa muda ambaye naye alimtambulisha mtangazaji wa kike mwenye kipaji kikubwa na cha kipekee cha kucheza 'Dancing', Feven Reuben maarufu kama Fevushka ambaye atakuwa akitangaza naye.

Mtangazaji huyo wa kike anaungana na Tbway kuunda timu mpya ya watangazaji wa 5SELEKT, kipindi ambacho kina lengo la kuwateka vijana kupitia burudani huku wakiwapa michongo mbalimbali, namna ya kutumia vitu vya kiteknojia pamoja na mada mbalimbali za mambo ya maisha ya vijana.

Uzinduzi wa kipindi hicho ulichagizwa na burudani kali kutoka kwa wasanii Angel Nyigu pamoja na Dayoo, wadau wao kutoka vyuoni walikuwa sehemu ya tukio hilo pamoja na washirika wa kibiashara wa EATV kutoka mtandao wa simu wa Airtel Tanzania na Serengeti Premium LITE.

Kipindi cha 5Selekt kina zaidi ya miaka kumi tangu kuanzishwa na kimekuwa jukwaa ambalo limewawezesha vijana wengi kufanikiwa ndoto zao, ikiwemo wasanii wakubwa na wanasiasa mbalimbali.

Moja ya viongozi hao ni Mkuu Wilaya ya Muheza, Zainabu Abdalah pamoja na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Jokate Mwegelo.



Watangazaji wa 5Selekt, Tibway 320 na Fevushka.

## KMC kutumia uwanja wao Ligi Kuu msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imetangaza rasmi kuwa itautumia uwanja wake wa nyumbani, KMC Complex, uliopo Mwenge, Dar es Salaam, katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku amesema kwa sasa upo katika hatua za mwisho za matengenezo, ikiwemo kuwekwa nyasi bandia, ambapo itahama Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ambao ilikuwa inautumia kwa miaka yote tangu ipande Ligi Kuu.

Chukuchuku alisema moja ya malengo ya kufanya vyema katika ligi msimu ujao ni kuutumia uwanja huo ambao anaamini utafanya wachezaji wa timu hiyo kuhisi wapo nyumbani, tofauti na inapocheza Uhuru.

"Tunataka msimu ujao tumalize kwenye nafasi nne za juu na moja ya mikakati yetu mbali na kusajili vizuri, lakini ni kuhakikisha tunacheza mechi zetu za nyumbani kwenye uwanja wetu, KMC Complex, ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika, tayari nyasi za bandia zimeshatandazwa, nakuhakikishia kama tutacheza hapa kwetu, tutashinda mechi nyingi zaidi kwa sababu wachezaji watajihisi wapo nyumbani, tofauti na Uwanja wa Uhuru," alisema Ofisa Habari huyo.

Kuhusu maandalizi ya msimu ujao, alisema kwa sasa wanasubiri mapendekezo ya mwalimu, Abdihamid Moalin ili kuhakikisha wanampatia kile anachohotaji.

## Dilunga afunguka kuibakisha JKT Tanzania Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

WINGA na kiungo mashambuliaji wa JKT Tanzania, Hassan Dilunga (pichani), ameeleza furaha yake kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu Tanzania Bara, akisema inabidi sasa wao kama wachezaji na viongozi kujipanga vyema kwa msimu ujao kwani utakuwa mgumu kuliko huu.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mechi ya 'play off' kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam dhidi ya Tabora United, Dilunga alisema haikuwa kazi rahisi kuibakisha timu hiyo hasa katika michezo miwili ya mchujo, ambayo walicheza kimkakati na malengo.



Katika mechi hiyo ya juzi, JKT Tanzania ililazimishwa suluhu uwanja wake wa nyumbani dhidi ya Tabora United, lakini ikibaki Ligi Kuu kutokana na ushindi wa mabao 4-0 iliyoupata Jumanne iliyopita, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora kwa mabao ya Said Ndemla, Ismail Aziz, Matheo Antony, na Hassan Dilunga mwenyewe.

"Tunashukuru tumebaki Ligi Kuu, lakini hatuna furaha sana kwa sababu malengo yetu hayajatimia.

Ilikuwa ngumu sana kubaki, lakini sisi tulijipanga kwa ajili ya mechi ya kwanza kabisa tumalize mechi kule kule, nguvu na kila kitu tulizitumia kule ndiyo maana tukapata matokeo mazuri ya mabao manne, hapa tulikuja kukamilisha ratiba tu," alisema.

Akiizungumzia ligi kwa ujumla alisema ilikuwa ngumu, hivyo wanapaswa kujipanga vizuri zaidi kuelekea msimu ujao

"Ligi ilikuwa ngumu kwa sababu JKT Tanzania ilikuwa msimu wake wa kwanza, tulidhani itakuwa ni kawaida lakini kumbe timu zilijipanga sana kufanya vyema msimu huu, kwa hiyo inatutahadharisha kuwa msimu ujao tujipange vizuri ili kupata matokeo mazuri," alisema.

Baada ya kufungwa, Tabora United itatarajia kujaribu tena habati yao ya kubaki Ligi Kuu, itakapocheza mechi ya kwanza ya 'play off' dhidi ya Biashara United, Jumatano, Uwanja wa Karume, Musoma, Mkoani Mara.

## ZISIKUPITE

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imewasilisha dau la pauni milioni 16 kwa Burnley kumnunua mlinda mlango wa England, James Trafford mwenye miaka 21, lakini Clarets wanataka pauni milioni 20. ***(Mail)***

### BRANTHWAITE HUYO MAN

MANCHESTER United inatarajia kukamilisha dili la kumnunua beki wa Everton, Jarrad Branthwaite kabla ya Juni 30 baada ya kiungo huyo kuachwa nje ya kikosi cha England cha Euro 2024 ***(Liverpool Echo)***

### NEVES OFA MPYA

MANCHESTER pia wanajiandaa kuwasilisha ofa ya pili kwa kiungo wa Benfica, Joao Neves, 19, baada ya ofa ya awali kukataliwa. ***(A Bola)***

### ALVAREZ KUBAKISHWA

KLABU ya Manchester City inataka kumbakisha mshambuliaji wa Argentina, Julian Alvarez na hawatapokea ofa zozote za mkopo kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Fabrizio Romano)***

### ATLETICO NA JULIAN

KLABU ya Aletico Madrid imekuwa ikihusishwa na Julian Alvarez, lakini rais wa klabu hiyo, Enrique Cerezo amesema haamini kuwa mshambuliaji huyo ataondoka pale Etihad. ***(Standard)***

### POTTER ATAKIWA

KLABU ya Leicester City imefanya mawasiliano na kocha wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter kuhusu nafasi yao ya ukocha. ***(Telegraph)***

### BAYERN YAMTAKA PALHINHA

KLABU ya Bayern Munich imefufua tena mazungunzo na Fulham kuhusu kumnunua kiungo wa kati wa Ureno Joao Palhinha mwenye miaka 28. ***(Sport)***

### NDOMBELE KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele, 27, anatazamiwa kuondoka Tottenham Hotspur kama mchezaji huru msimu huu wa joto. ***(Foot Mercato)***

### SILVA ALENGWA

KOCHA wa Fulham, Marco Silva anaweza kuwa kwenye mipango ya Nottingham Forest iwapo kocha wao, Nuno Espirito Santo ataondoka kwenye klabu hiyo. ***(Mail)***


### TEN HAG ATETEWA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal amesema kuwa kocha mwenzake wa Uholanzi, Erik ten Hag hatakiwi kufutwa kazi na klabu hiyo ya Ligi England. ***(Metro)***

### ONANA AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Everton, Mbelgiji Amadou Onana mwenye miaka 22 ana matamanio ya kujiunga na klabu ya Arsenal. ***(Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ALEXIS MAC ALLISTER HAONDOKI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

**Nyota huyo amefichua kile alichoelezwa na kocha anayeondoka Liverpool, Klopp kuwa ni...**

ALEXIS Mac Allister amefichua kuwa Jurgen Klopp alimtaka aendelee na maisha yake ya soka katika klabu ya Liverpool wakati akikiaga kikosi hicho msimu huu wa joto.

**Klopp alijiuzulu mwishoni mwa msimu huu uliopita baada ya kujenga urafiki mkubwa na Mac Allister, ambaye alisajiliwa kutoka Brighton & Hove Albion wakati wa dirisha dogo.**

Mac Allister alicheza mechi 46 katika mashindano yote, ni Virgil van Dijk na Luis Diaz pekee waliocheza dakika nyingi zaidi katika kipindi chote cha kampeni ya ubingwa na Muargentina huyo alikiri kukatishwa tamaa kwa Klopp kwa kukosa kufanya kazi kwa muda mrefu pamoja.

"Wakati fulani tulikumbatiana na aliniambia kuwa ilikuwa ni aibu kwamba tulikuwa tumeshiriki mwaka mmoja tu, lakini ilinipa imani kubwa kwa siku zijazo," Mac Allister aliambia TyC Sports.

"Aliniambia nipo kwenye klabu sahihi.

"Kila kitu kinafanya kazi vizuri kwa Liverpool, sio klabu yenye majigambo makubwa na kila mtu anajaribu kukusaidia kadri awezavyo.


"Uwanjani kila kitu ni tofauti, kwa sababu kila kitu kinaweza kuwa kizuri sana nje, lakini lazima ufanye vizuri uwanjani. Nimelazimika kucheza nafasi mbalimbali na nilifurahia sana, nafurahi kuwa kwenye klabu kubwa kama Liverpool."

Mac Allister amejikuta akizungumziwa kuhusu uhamisho wa wachezaji msimu huu, huku ripoti nchini Argentina zikipendekeza kipengele cha "siri" cha pauni milioni 60 cha kumuachilia kimemwacha machoni pa Real Madrid.

Baadaye ilifichuka kwamba Liverpool hairuhusu vifungu vya kutolewa katika mikataba ya wachezaji wao.

Mac Allister ameweka wazi kuwa hana nia kuondoka Liverpool msimu huu wa majira ya joto na kocha mpya Arne Slot atakuwa na nia ya kufanya kazi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye kwa sasa yuko na Argentina kwa ajili ya michuano ya Copa America.

# ZIDANE AMTABIRIA MAKUBWA MBAPPE REAL MADRID




**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema Kylian Mbappe ataweka historia katika klabu ya Real Madrid, huku mshambuliaji huyo wa kiwango cha kimataifa akitarajiwa kuwasili Uhispania mwezi ujao.

Baada ya sakata la muda mrefu la uhamisho, Mbappe hatimaye aliweka bayana kujiunga na Madrid ambapo atatua rasmi kwa mabingwa hao wa Ulaya baada ya Euro 2024.

Mashabiki tayari wanatazamia siku za usoni kumuona Mbappe na Zidane hakuficha furaha yake katika mahojiano ya hivi majuzi na Telefoot.

"Mbappe yuko hapa sasa," alisema Zidane.

"Ataweka historia katika klabu na nadhani atampita kila mtu."

Zidane alitumia miaka mitano kama mchezaji ndani ya Madrid kabla ya kuwa kocha kati ya mwaka 2016 na 2021, alikuwa na kumbukumbu nzuri za wakati wake akiwa na usukani wa wababe hao wa Hspania.

Alipoulizwa ni wachezaji gani waliomvutia zaidi kama kocha Zidane aliambia Canal+: "Unapowaona Toni Kroos, Luka Modric na Karim Benzema wakicheza kwa ajili yako kwa saa moja bila kupoteza mpira hata mmoja, hiyo ni soka."

Zidane pia alipasifia Santiago Bernabeu kama uwanja mzuri zaidi kuwahi kuchezea, akikiri kwamba nyumba ya Madrid ni "ya kipekee kabisa".

Mbappe tayari ametokea Bernabeu mara tatu katika maisha yake ya soka, huku akishindwa mara mbili kwa 3-1 na sare ya 2-2 akiwa na PSG, alipokelewa kwa furaha na mashabiki wa nyumbani Machi 2022 wakati ilitarajiwa angejiunga na Los Blancos majira hayo ya joto.

# Silva amtaka Neves City

**MANCHESTER,** England

BERNARDO Silva amekiri kuwa anataka mchezaji anayelengwa na Manchester United, Joao Neves ajiunge naye Manchester City.

Neves amekuwa akihusishwa sana na kutaka kuondoka Benfica majira ya kiangazi, huku United ikisemekana kuwa miongoni mwa klabu zinazoongoza kumtaka.

Mkataba wake una kipengele cha kutolewa chenye thamani ya takriban pauni milioni 100.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 amepiga hatua kubwa mapema katika maisha yake ya soka na hata kupata nafasi katika kikosi cha Ureno kitakachoshiriki Euro 2024.

Akizungumza na O Jogo wiki hii, Silva alifichua kuwa angemshauri Neves kusaini City badala ya United ikiwa nafasi hiyo itatokea.

"Ningemwambia aende Manchester City," Silva alijibu alipoulizwa kuhusu nia ya United kwa Neves.

"Siyo rahisi. Ni mchezaji ambaye, kutokana na mafanikio yake msimu uliopita, ana klabu nyingi zinazomtaka. Kama Mreno na mchezaji ninayempenda, ningependa kumuona akiwa pamoja nami."

Aliongeza: "Sihitaji kumshawishi Pep Guardiola, Joao Neves tayari anashawishi, kwa jinsi anavyofanya kazi, kwa nguvu anayoleta kwenye mchezo.

Itakuwa rahisi kwa klabu nyingi kuingia kwenye mbio na afanye uamuzi wake, iwe bora kwake ikiwa ataendelea na nguvu hii, ana mustakabali mzuri sana mbele yake.

Neves ameichezea Benfica michezo 75 ya wakubwa hadi sasa katika maisha yake ya soka na kuisaidia kushinda mataji mawili tangu alipoanza kucheza mwaka 2023.




# *Martinelli ampigia chapuo Vinicius*



**LONDON,** England

WINGA wa Arsenal, Gabriel Martinelli amesema yupo nyuma ya Mbrazil mwenzake Vinicius Junior katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Ballon d'Or.

Vinicius ni miongoni mwa wanaopigiwa upatu mapema kushinda tuzo hiyo msimu huu wa majira ya joto baada ya kung'ara akiwa na Real Madrid waliotwaa ubingwa wa LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini anakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa mchezaji mwenzake Jude Bellingham ikiwa anataka kutwaa tuzo hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Martinelli alisisitiza Vinicius ndiye mshindi anayestahili wa tuzo ya kifahari ya Ballon d'Or.

"Bila shaka, ni fahari kubwa kucheza naye," alisema.

"Kupitia maisha ya kila siku, kumuona yeye ndiye anayestahili. Nina furaha sana kuwa Mbrazil na kuona Vini aking'ara.

"Kwa maoni yangu, anastahili kushinda Ballon d'Or."

Vinicius pia amepata uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa mastaa wa Brazil Rivaldo na Ronaldo, ambao walimtaja winga huyo wa Madrid kama "mchezaji bora zaidi duniani".

"Yeye ni mvulana anayejitolea sana," Rivaldo aliiambia ESPN.

Alifika Real Madrid na kwenda Real Madrid B kujifunza. Alicheza mechi chache na tuliweza kuona kwamba bado alihitaji muda kidogo kujifunza jinsi ya kufunga.

Na alijifunza! Alifanya mazoezi kwa bidii na kujitolea. Leo hii unaweza kuona kwamba ana wakati rahisi zaidi wa kufunga.

"Kwa hiyo Vini ni mchezaji wa kupongezwa. Anastahili Ballon d'Or. Bila shaka, hakuna kitu bora kwake zaidi ya kupata tuzo hiyo mara moja na kwa wote kuliko kushinda Copa America.

"Leo tayari anastahili tuzo hiyo, lakini kama atashinda Copa America itakuwa bora zaidi."

## HABARI MICHEZO

## Yanga yatenga bilioni 24/-

INATOKA UKURASA 24

hakuna linaloshindikana," alisema Msigwa.

Vile vile aliwataka wanachama wa klabu hiyo kuepuka migogoro kwani inaharibu maendeleo ya michezo na kusema kwenye migogoro hakuna mafanikio.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Baraza la wadhamini wa klabu hiyo, George Mkuchika aliitaka Kamati ya usajili iwe makini kwenye kufanya usajili wa wachezaji ili waendelee kufanya vema msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano ya Kimataifa.

Kwa upande wa Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za mitaa Tamisemi, Muhamed Mchengerwa alisema Serikali imekubali kutoa eneo la kujenga uwanja wa kisasa kwenye mradi wa bonde la mto Msimbazi.

"Tayari tumepokea zaidi ya bilioni 400 kutoka kwa Rais Samia akitaka tuimarishe kingo za mto huo, ninaahidi kuwapa eneo mnalolitaka endapo mtashindwa kufuata michoro na vigezo mtakavyopewa nitawapokonya," alisema Mchengerwa.

Alisema Serikali imejizatiti kutengeneza vijana kupitia mashindano mbali mbali na kuweza kupata wachezaji watakaounda timu ya Taifa watakaotumika miaka ijayo.

## Simba yatua Mali kusajili

INATOKA UKURASA 24

vya chini," kilisema chanzo hicho.

Inadaiwa safari hii Dewji mwenyewe yupo mstari wa mbele katika kusajili wachezaji wa viwango vya hali ya juu, akiwaongeza watu wengine kumsaidia kazi hiyo ambao ni Sued Mkwabi, Mulamu, Ng'ambi, Crescentius Magori na Kassim Dewji.

Meneja Habari wa Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally alisema mipango yote inatekelezwa kwa ustadi na ufanisi wa hali ya juu.

"Usahihi ni kwamba mipango na mikakati thabiti inaendelea na itakapokua tayari wote watajulishwa.

Jambo la kufurahisha ni kwamba mipango yote inatekelezwa kwa ustadi na ufanisi wa hali ya juu mno, malengo tuliyojiwekea ya kuboresha timu yetu yamefikiwa kwa asilimia kubwa kwa maana ya kwamba mipango yetu kwenye soko la usajili iko vizuri sana.

Niwaombe wanasimba tutulie, la mgambo likilia tutafahamu kila kitu kuhusu timu yetu pendwa," alisema Ahmed.

# NAMUNGO: TUMEONA PANAPOVUJA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo FC, imesema tayari wameshajua makosa waliyoyafanya msimu uliopita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na hawatoyarudia msimu ujao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Idrissa Bandari amesema kwao msimu uliomalizika hivi karibuni haukuwa bora sana, wala mbaya sana, lakini walikuwa nje ya malengo waliyojiwekea ya kumaliza katika nafasi nne za juu kitu ambacho kimeshindikana.

**Alisema kutokana na kumaliza kwenye nafasi ya nje ya malengo yao, wamejipanga kuhakikisha wanarudi kwa nguvu mpya, na kwa bahati nzuri wameshajua nini kilikwakwamisha.**

"Tumejifunza kutokana na makosa, tumejua nini tumekifanya na kusababisha tutoke nje ya malengo ya klabu. Kwa sasa menejimenti inaandaa timu ili tuwe na kikosi bora msimu ujao, wanamalizia kusoma ripoti ya mwalimu ili sasa tuanze kufanyia kazi, hasa upande wa usajili," alisema Bandari.

Akitoa tathmini ya msimu uliopita wa kikosi hicho chenye maskani yake Lindi, alisema walikuwa na vipindi vinavyobadilika, kushuka na kupanda, kitu kilichosababisha kumaliza ligi ikiwa nafasi ya sita, kwa kuwa na pointi 36.

"Msimu uliomalizika, haukuwa bora sana, wala haukuwa mbaya sana, hatukuanza vizuri karibia mechi tano za mwanzo, katikati ya msimu tukafanya vizuri sana, lakini kuelekea mwisho wa msimu hatukuwa vizuri pia, hadi tulipogeuka tena mechi chache za mwisho tukashinda.

Malengo yalikuwa tuwe ndani ya nne bora, lakini tumeikosa kwa hiyo tumemaliza nje ya malengo ya klabu tuliyojiwekea, tutarekebisha haya yote msimu unao", alisema.



Mchezaji wa mchezo wa Gofu, Foti Gwebe Nyirenda, akipiga mpira wakati wa michuano ya 13 ya mchezo huo iliyoandaliwa na Klabu ya Rotary Bahari ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## *Tamasha Utamaduni, Utalii Kanda ya Ziwa lazinduliwa*

**Na Jumanne Juma**

TAMASHA kubwa la kimataifa la Utamaduni na Utalii linalojulikana kama 'Lake Zone Cultural and Tourism Festival' limezinduliwa rasmi jana jijini Dar es Salaam huku likilenga kuwafikia washiriki wengi zaidi.

Tamasha hilo linaloandaliwa limepangwa kufanyika mapema mwezi ujao Bariadi, Mkoani Simiyu.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo uliohudhuriwa na maofisa kutoka Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Mratibu wa tamasha hilo, Christina Emmanuel, alisema hii mara ya kwanza kuratibu tamasha hilo lakini wamejipanga liwe la kimataifa kwa kuwa na vivutio vingi zaidi.

"Tamasha hili linatarajiwa kufanyika mwezi wa saba na ninayo furaha kuwafahamisha kuwa litafanyika kwa siku tatu mfululizo kuanzia Julai 5 na kilele chake kitakua Julai 7 ambapo pamoja na mambo mengine tunategemea kuwa na maonyesho mbalimbali ya masuala ya utamaduni na utalii katika Uwanja wa Halmashauri na kuwavutia washiriki na watazamaji zaidi ya 7000 kwa siku hizi tatu," alisema.

Aliongeza kuwa tamasha hilo litakuwa na vionjo mbalimbali ikiwemo ngoma inayohusisha makabila ya Wagika na Wagulu, maonyesho, michezo mbalimbali na vyakula Aidha, Mkurugenzi wa kampuni inayoandaa tamasha hilo, Mohamed Hatibu alitoa wito kwa wafanyabiashara , makampuni , taasisi na mashirika kujitokeza na kuunga mkono tamasha hilo kama njia moja wapo ya kukuza utalii na kutangaza tamaduni za Tanzania.

"Tumejiandaa vizuri na tuna uhakika tamasha hili litafanikiwa na litakuwa la kila mwaka,"alisema Hatibu.

Aidha, Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji na Maendeleo ya Sanaa wa BASATA, Edward Buganga alisema baraza hilo lina furahia juhudi za waandaaji wa tamasha hilo katika kukuza sanaa na utamaduni wa watanzania.

"Ni tamasha kubwa la aina yake ambalo sisi kama Watanzania tunapaswa kujivunia kuwa hili ni tamasha la kwetu kwa maendeleo ya utamaduni na utalii wetu,"alisema na kusisitiza kuwa Basata itatoa ushirikiano mkubwa kwa waandaaji ili tamasha hilo lifanyike kwa ufanisi mkubwa.

# Michezo

Jumatatu Juni 10, 2024

Nipashe



Zidane amtabiria makubwa Mbappe UKURASA 22

# Yanga yatenga bilioni 24/- kujiendesha msimu ujao

●●● Zitatumika pia kwenye usajili kwa ajili ya maboresho ya timu...

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Yanga imetangaza kutenga kiasi cha shilingi bilioni 24.5 kama bajeti ya msimu ujao kwa ajili ya usajili na kujiendesha.

**Akizungumza kwenye Mkutano Mkuu jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Fedha wa klabu hiyo, Sabri Sadick, alisema anaimani kupitia bajeti hiyo watapata mafanikio msimu ujao.**

"Hii ni bajeti ambayo tumeipanga kwa ajili ya msimu ujao na imewasilishwa kwa uongozi wa juu kwa utekelezaji na mipango mingine," alisema Sadick.

Kwa upande wake, Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said alithibitisha kupokea bajeti hiyo na kuweka wazi kuwa Yanga inapaswa kujengwa kiuchumi ambapo kutokana na juhudi wanazozifanya wamefanikiwa kupata idadi kubwa ya wadhamini.

"Kupitia fedha za wadhamini wetu tumepata mafanikio makubwa, mpaka sasa tumepata mafanikio mengi, tunaahidi kuendelea kuwapa thamani kwa kufanya vizuri kwenye michezo yetu yote ya ndani na ya Kimataifa," alisema Hersi.

Aidha alisema katika kuhakikisha wanapata mafanikio zaidi watafanya usajili bora hasa wa kimataifa kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu pamoja na kuboresha benchi lao la ufundi ili kuwa bora zaidi ya msimu uliopita.

Aliongeza kusema kuwa wamepata mialiko kutoka nchi za Afrika Kusini, Kenya, Uganda pamoja na nchi moja ya Ulaya ambayo aliahidi kuitaja hapo baadae kwa ajili ya kwenda kuweka kambi kujiandaa na msimu ujao.

"Tumepokea mialiko kutoka nchi hizo pamoja na nchi moja ya Ulaya zikituomba kwenda kuweka kambi kwa ajili ya maandalizi yetu ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na michuano ya kimataifa, tunaendelea kuifanyia kazi mialiko hiyo na muda ukifika tutatoa taarifa," alisema Hersi.

Katika hatua nyingine, Hersi aliwatangazia wanachama kuwa wamepeleka barua Serikalini kuomba wapatiwe eneo kwenye mradi wa bonde la mto msimbazi ili waweze kujenga uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu.

"Tumeandika barua ya kuomba Serikali itupe eneo kwenye mradi wa bonde la mto Msimbazi ili tuweze kujenga uwanja wa kisasa ambao utaongeza thamani ya klabu yetu na kutufanya tuwe bora zaidi," alisema Hersi.


Pia alisema watafanya jitihada kuhakikisha wanaendeleza timu ya vijana pamoja na ile ya wanawake (Yanga Princess) zizidi kuwa bora na kuwafungulia njia wanawake kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

"Niwaombe wanachama mtuunge mkono kwa kulipia kadi za uwanachama ili tuweze kufikia malengo na kupata maendeleo zaidi," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa alipongeza uongozi wa Klabu hiyo kwa kufanya kazi kiuweledi.

"Mafanikio ya Yanga yametokana na uongozi bora wenye kufanya kazi kwa weledi, kutokana na ubora mliokuwa nao natamani kuona timu hii inakuwa kama Manchester

INAENDELEA UKURASA 23



Rais wa Yanga, Hersi Said

## Simba yatua Mali kusajili mshambuliaji

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba tayari imeanza mikakati ya kukiimarisha kikosi chao kwa kuamua kwenda nchini mali kusajili mshambuliaji atakayewasaidia kuwarudisha kwenye ubora wao.

Simba inatajwa kutaka kumsajili mshambuliaji wa klabu ya FC Nouadhibou ya Mauritania raia wa Mali, Ibrahim Gadiaga.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mshambuliaji huyo amepachika mabao 12 kwenye Ligi Kuu ya Mali akiwa na klabu ya Bakaridjan kabla ya kuhamia nchini Mauritania na kujiunga na klabu hiyo.

"Bado waliopewa dhamana ya kusajili wanahaha huku na kule kusaka mshambuliaji mwenye uwezo mkubwa na siyo kama wale waliokuwapo msimu uliopita, hivi sasa wamekwenda mpaka Mauritania kuulizia uwezekano na kumpata kijana huyu raia wa Mali, ana miaka 19 tu, lakini analijua goli, kama wakifanikiwa na kumpa mkataba mrefu anaweza kuisaidia Simba kwa muda mrefu," kilisema chanzo ndani ya klabu hiyo.

Aidha, taarifa zinasema kuwa tayari kikosi kazi kilichopewa mamlaka ya usajili na Mwekezaji, Mohamed Dewji, kinadaiwa kimeshakubaliana na winga anayeichezea klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Kongo, Elie Mpanzu na Derrick Fordjour kutoka Medeama ya Ghana.

Pia Simba inatajwa kumuwinda mshambuliaji Ricky Banda, raia wa Zambia anayeichezea Red Arrows ya nchini humo.

"Rais wa Heshima anataka kurudisha ufalme wa timu, ndiyo maana ameteua kikosi kazi, baada ya kuona kuna watu wanamkwamisha, anatoa pesa, lakini wanaletwa wachezaji wenye viwango

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >